ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe.Balozi Seif Ali Iddi - MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6. Mhe. Haji Omar Kheri - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo - MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume - MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma - MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed - MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico - MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib - MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/Nafasi za Wanawake

18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe.Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani

40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake

41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi

42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake

43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo

44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy - Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake

75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga

76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu

77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais

78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani

79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake

81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni

82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni

85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake

86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 16 Juni, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: namuomba kumwita Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili aiwasilishe.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika wakati mimi najibu swali 147 liliulizwa swali ya nyongeza na Mhe. Mohamed Said Mohamed alitaka kujua wizara inaweza kuliambia Baraza lako hili tukufu kiasi kilichofanywa na kusaidia wanavijiji husika aliyotaja katika Huba ya Menai.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo. Fedha za makusanyo ya Hifadhi ya Huba ya Menai zinatumika kusaidia shughuli mbali mbali za jamii kama vile mifuko ya maafa, matengenezo ya vyombo vya uvuvi, ununuzi wa mitego ya uvuvi na kadhalika. Aidha mafanikio ambayo tayari yamepatikana kupitia mapato ya Huba ya Menai ni kama ifuatavyo:

1. Ujenzi wa jengo la wavuvi Mtende - Kusini 5,548,300
2. Ujenzi wa soko Dimani - Magharibi 2,165,000
3. Ujenzi wa Msikiti Pungume - Magharibi 832,000
4. Umalizaji wa chumba cha kompyuta ya Skuli ya Bwefum - Magharibi 500,000
5. Uchimbaji wa kisima Kibwegele Kajengwa - Kusini 3,000,000
6. Mchango wa ujenzi wa soko Kizimkazi Dimbani - Kusini 6,491,664
7. Ujenzi wa jengo la kamati Dimani - Magharibi 2,070,000
8. Ujenzi wa banda la kuku Muyuni - Kusini 1,036,000
9. Ujenzi wa soko la samaki Kizimkazi Mkunguni - Kusini 810,000
10. Ujenzi wa vyoo vya msikiti Kizimkazi Dimbani - Kusini 1,002,000

Jumla ni 93, 054,964

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante waheshimiwa mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Simai Mohammed Said atafuatiwa na Mhe. Viwe Khamis na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis ajiandae, Mhe. Simai karibu sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, awali ya wote nichukuwe nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kuniona mimi lakini pia nikuombe tu Mhe. Spika, wakati nilikuwa naendelea kujitayarisha nilikuwa sijajipanga kwamba jina langu litakuwa leo la mwanzo asubuhi naomba uniondoe kwa hivi sasa halafu wakati namaliza kujipanga waanze watu wengine halafu kama muda utaruhusu na mimi utaweza kuniona kwa baadaye. Hayo ni maombi Mhe. Spika kwa heshima kabisa ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante nilimwita Mhe. Viwe.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii ya leo kwa kunipa fursa hii nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala ambaye ametupa uhai tukaweza kusimama hapa ndani ya Baraza hili tukufu na tukaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii niwatakie wananchi wa Zanzibar Ramadhan Karim ikiwa leo ni mwezi ishirini na moja.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wao mzuri kwa taarifa hizi na hotuba hii ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwenye ukurusa wa 28. Mhe. Spika, katika ukurasa hii kuna vipa umbele ambavyo kuwa Serikali wameviweka katika mwaka huu wa 2017/2018.

Mhe. Spika, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka vipa umbele hivi ambavyo kuwa vitawaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze na kipa umbele cha (a) Kuimarisha Ubora wa Huduma za Kijamii zikiwemo Elimu, Afya, Makaazi na Upatikanaji wa Maji safi na Salama.

Mhe. Spika, Serikali wasimamie kwa kina upatikanaji wa huduma hizi katika jamii tukiangalia tatizo la maji, tatizo la maji Zanzibar lipo na linasumbua na bado litaendelea kuwepo kwa hivyo tumuombe Mhe. Waziri au Serikali waliangalie kwa kina tatizo la maji, kwa sababu tatizo hili la maji limeenea katika majimbo yote ya Zanzibar.

Niende kwenye upande wa afya Mhe. Spika, leo tayari tupo tunaichangia bajeti hii tokea jana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini kuna changamoto ambazo kuwa zinajitokeza katika mawizara hasa tunapokwenda kwenye kamati zetu tunakuwa tunapata malalamiko katika Wizara kutokuingiziwa fedha kwa wakati. Kwa hivyo Mhe. Spika, niiombe Serikali wawaingizie mawizara fedha kwa wakati ili waweze kutatua zile changamato ambazo zinawakabili katika wizara yao.

Kwa upande wa Wizara ya Afya Mhe. Rais wa Zanzibar alitangaza huduma ya kinamama kuwa itakuwa bure lakini kutokana na kuwa fedha hizi ambazo kuwa zinaweza zikanunuliwa vifaa

zikaweza kuwasaidia kinamama kuwa hazitoki kwa wakati na hivyo husababisha changamato kubwa ya kinamama hawa wakati wanakwenda kujifungua ya kununua hivi vifaa ambavyo kuwa zinaweza vikatumika kipindi kile cha wakati wa kujifungua.

Mhe. Spika, kwenye Wizara ya Elimu mwaka jana walianza kutoa madaftari lakini kipindi hiki madaftari yalichelewa kutolewa kwa sababu ya kutokuingiziwa fedha za kununua madaftari kwa wakati, ili vijana wetu wakaweza kupatiwa madaftari haya kwa wakati.

Mhe. Spika, niiombe Wizara ambayo inashughulikia utoaji wa fedha hizi basi fedha hizi zitolewe kwa wakati ili vijana wetu waweze kupatiwa madaftari kwa wakati.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwa ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ilani yake vizuri na kuweza kuisimamia Serikali vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar alisema katika ilani yake kuwa atawaongezea wafanyakazi wa kipato cha chini mshahara, nimpongeza Mhe. Rais kwa kutekeleza ahadi yake hii na hivi sasa tumeona matunda yake kwa wafanyakazi ambao kuwa aliwaahidi kuwa atawatekelezea ahadi hii au azma hii.

Mhe. Spika, pia niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwapelekea wananchi wa Kisiwa cha Fundo huduma ya umeme pamoja na mpango wake wa kutaka kuwapelekea huduma ya umeme wananchi wa Kisiwa cha Kokota. Kisiwa hiki cha Kokota Mhe. Spika, kipo katika Jimbo la Mtambwe.

Mhe. Spika, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwapelekea wananchi hawa kisiwa cha Kokota huduma hii ya umeme katika mwaka huu 2017/2018.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa 38 umalizwaji wa madarasa ambayo kuwa yamejengwa kwa nguvu za wananchi, Mheshimiwa nimeiona katika bajeti hii au hotuba hii ya Mhe. Waziri kuwa kumetengwa pesa ambazo kuwa zitamaliza mabanda haya ambayo kuwa yamejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mhe. Spika, niipongeze Serikali kwa kuweka kiwango hiki ambacho kuwa kitaweza kumaliza madarasa haya ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mhe. Spika, niseme kuwa kina changamoto kubwa katika maskuli yetu hasa katika Kisiwa cha Pemba, kuna madarasa mengi ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi lakini mpaka leo hii madarasa haya hayajaezekwa, na husababisha wanafunzi wa madarasa matatu kukaa katika chumba kimoja.

Mhe. Spika, wanafunzi hawa ambao wanakaa katika chumba kimoja wanafika madarasa matatu elimu kabisa haiwezi kupatikana, kwa sababu hata mwalimu anashindwa kusomesha na ndio pale tunapoona vijana wetu wanafeli kutokana na uhaba wa madarasa ya kusomeshea vijana wetu hawa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nichukuwe fursa hii nimpongeze tena Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mpendae Mhe. Dimwa pamoja na wajumbe wake wote, mwisho niseme kwa niaba ya vijana Mkoa wa Kaskazini Pemba na wanawake wote wa Zanzibar naunga mkono hutuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Viwe naomba sasa nimwite Mhe. Mwantatu atafuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi kuweza kuchangia bajeti hii kuu ya Serikali.

Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa umakini wake na usimamizi wake bora katika wizara hii muhimu kwa maslahi yetu sote.

Mhe. Spika, pia napenda kuwapongeza viongozi na watendaji wote wa wizara hii kwa juhudi zao wanazozichukuwa katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku, juhudi hizi ndizo zilizopelekea leo hii sisi wajumbe wa Baraza lako hili tukaweza kukaa na kujadili bila ya juhudi zao nafikiria tusingeweza kupata kitabu cha kuweza kukujadili leo hii.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika mchango wangu, mchango wangu nianzae kuzungumzia suala zima la mfumumko wa bei ambao umezungumzwa katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, mfumuko wa bei ni changamoto kubwa katika Serikali yetu kila uchao bei zinapanda tafiti nyingi zimefanywa lakini vile vile vikao vingi vimefanyika na wafanyabiashara vile vile Serikali inajitahidi kupunguza kodi kwa wafanyabiashara, lakini bado suala hili halijapata ufumbuzi wake.

Mhe. Spika, kwa mawazo yangu mimi nahisi muarubaini wa suala hili ni kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha tunajikita katika uzalishaji wa ndani.

Mhe. Spika, tunaweza kuwekeza katika kilimo ili kupunguza gharama kubwa ndani ya Serikali yetu, Serikali imejipanga vizuri lakini nahisi bado mikakati madhubuti haijachukuliwa.

Mhe. Spika, mimi ninavyokumbuka zamani kulikuwa na mikakati wakati mimi niko mdogo nikishuhudia wafanyakazi wa kilimo wakichukuliwa magari kwa magari wakipelekwa katika maeneo ili kuhakikisha mashamba yale ya Serikali yanalimwa na kupata mazao mengi. Lakini mbali ya hivyo katika vile vituo vya kilimo kumbukumbu zangu zilikuwa zinanionesha, katika kituo cha Bungi pale palikuwa mwezi kama huu wa Ramadhani mihogo inavunwa magari kwa magari na inasambazwa kwa wananchi na kwa kipindi hicho kuliwa hakuna tabu ya vyakula kama kipindi hiki, cha kushangaza wakati huu hakukuwa na miradi mingi ambayo wafadhili wanakuja kuwekeza katika sekta ya kilimo. Lakini sasa hivi kuna miradi mingi ambayo wafadhili wa nje wanakuja kuwekeza na Serikali inapanga lakini manufaa yake naona hayako vizuri tofauti na zamani, sijui changamoto ni nini lakini mimi ninavyohisi kwamba bado hatujawa na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunawekeza katika kilimo ili kuepukana na huu mfumko wa bei lakini vile vile kurahisisha maisha kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, lakini vile vile tunaweza kuwekeza katika uvuvi katika suala hili lazima hapa tujitahidi kuongeza jitihada za kuimarisha sekta hii ya uvuvi, lakini vile vile kuweka mazingira mazuri katika sekta ya uvuvi ili tukaweza kuboresha huduma hii na tukaweza kuwepukana na huo mfuko wa bei. Kwa sababu Mhe. Spika hivi sasa hapa kwetu tuna wavuvi wengi tu na tukitazama kisiwa chetu kimezungukwa na bahari hakuna sababu ya kwamba sisi sasa tununuwe samaki ambao wanaletwa kwenye makotena lakini hapa niweze kusema kwanza bado Serikali haijajipanga vizuri, zaidi tunaangalia kusimamia katika uvuvi wa ndani. Wavuvi wetu wadogo wadogo wanavua katika uvuvi wa ndani, uvuvi wa ndani hivi sasa hivi wavuvi wanaambiwa wasivue wasivuwe uvuvi wa ndani kwa kuhifadhi matumbawe.

Lakini sasa uwezo wa kwenda bahari kubwa hawana kwa hiyo ili tuwe vizuri katika hii sekta ya uvuvi mimi nashauri turejeshe ile hali ya zamani, zamani nakumbuka kulikuwa kuna maduka ya *fisheries* yale Ramadhani kama hii hatupati shida lakini vile vile kulikuwa na magari pia *fisheries* wanavua walikuwa na mameli wanavua na tulikuwa hatuna shida ya vitoweo. Lakini sasa hivi kuna shida kubwa Zanzibar tumezungukwa na bahari lakini bado watu wanakula vyakula vikavu, wengine samaki yanayoletwa kwenye mafriji hawawezi kuyala na uvuvi wa kwetu hapa wavuvi hawana uwezo wa kuvua samaki wengi. Kwa hivyo mimi nahisi hapa tungerejesha tukakaa tukaandaa mikakati tukarejesha ile hali ya zamani ikawa *fisheries* pia wanajikita katika suala zima la uvuvi, na si kuratibu tu masuala ya uvuvi na matumbawe na mazingira na mambo mengine zaidi wajikitie katika kuhakikisha vipi tunaweza kuwanufaisha wazanzibari katika suala zima la uvuvi.

Mhe. Spika, hali kadhalika nije katika suala zima la ufugaji, tunaweza kuepukana na huu mfumko wa bei au kupambana na hii changamoto ili kuwekeza katika sekta ya ufugaji tukajenga mazingira mazuri ambayo wafugaji wetu wakaweza kufuga vizuri na tukaweza kupata maslahi.

Mhe. Spika, kwa takwimu ndogo tu nilizonazo na utafiti mdogo tu Zanzibar tuna mahitaji ya tani 65,000 kwa mwezi, na uzalishaji wetu wa ndani ni tani 15,000 kwa mwezi. Hii ni *gape* kubwa sana kwa hiyo lazima hapa tujitahidi kuimarisha mpango huu ili tuweze kufikia yale matakwa yetu. Mhe. Spika, maeneo yote haya endapo tutayawea mikakati madhubuti basi kuna mwelekeo mkubwa wa kupunguza mfumko wa bei, lakini vile vile kukuza pato letu la taifa.

Mhe. Spika, lakini katika suala zima la uwekezaji katika kilimo, serikali inategemea kuwa na mradi mkubwa wa *irrigation*, *solution* ya yote haya katika kilimo tuwe na kilimo cha umwagiliaji. Kilimo hiki kitatusaidia sisi katika kuekeza kwa kupata chakula cha kutosha katika nchi yetu, vyenginevyo tutakuwa tunaimba tu kwa sababu hali halisi tunaiona jua linakuwa kali sana na kwa kutegemea mvua na hiyo mvua yenyewe ikiwa nyingi pia huwezi ukalima. Kwa hiyo, muarubaini wake ni huu mradi tufanye jitihada ili tufanye haraka uweze kutekelezwa ili kuepukana na hayo.

Mhe. Spika, nije katika kitabu hiki kwenye suala zima la ugatuzi wa madaraka. Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kutekeleza azma hii, suala la ugatuzi wa madaraka ni suala la msingi kwani dhana hii ya ugatuzi wa madaraka utawawezesha wananchi kuamua nini hitaji lao. Kwa hiyo, madaraka haya yanakwenda moja kwa moja kwa wananchi kule chini.

Mhe. Spika, lakini nimeona katika kitabu hiki kwamba kuna sekta tatu ambazo zimegatuliwa, sekta ya elimu, sekta ya kilimo na sekta ya afya. Lakini katika kitabu hiki ukurasa wa 35, kifungu cha 74 kinaeleza kwamba yale mahitaji tuseme katika elimu, elimu ya msingi na ya maandalizi zimepelekwa huku chini Mikoani. Lakini kinachonipa wasiwasi ni kwamba yale madaftari na chaki yaani yale manunuzi ya vifaa vya kusaidia elimu kuipeleka mbele yote yatafanywa na Wizara ya Elimu. Mimi wasiwasi wangu ni kwamba hapa haya madaraka tumeshawapa watu wawili, kwa hivyo mwisho wa siku nani tutakuja mshika hatuombi tuharibikiwe, tunaomba twende vizuri lakini endapo mambo yakiwa mabaya nani atajibu, kwa sababu tumepeleka madaraka Mikoani lakini madaraka yenyewe yako nusu nusu. Mheshimiwa mimi pendekezo langu katika hili halikadhalika nimeona katika kilimo masuala ya pembejeo yote yatatoka Wizara ya Kilimo, lakini huku tumeshapeleka ugatuzi. Pia katika afya masuala ya ununuzi wa madawa kila kitu yatatoka Wizara ya Afya, huku tumeshawagatua.

Mimi nahisi hapa kidogo serikali labda Mhe. Waziri atapokuja aniweke sawa, lakini mimi napata mashaka mwisho wa siku endapo katika afya kule wakisema aah sisi hatukuweza kufanya hivi kwa sababu ya huku, na huku wakasema aah sisi hatukuweza kwa sababu hawa hawakutuletea mapema itakuwa hatuna nani wa kumshika. Mimi ningependekeza kwamba kama tunagatua basi tugatuwe na kila kitu chake tupeleke kule. Kwa hivyo, mwisho wa siku sisi tutajua nani tunamkamata.

Mhe. Spika, nije katika sekta ya afya. Sekta ya afya, sekta zote ni muhimu lakini kuna na muhimu zaidi kwa sababu afya ndio kila kitu bila ya afya hatuwezi sisi tukasimama hapa na kuweza kuzungumza kama hivi tunavyozungumza. Lakini vile vile bila ya afya hatuwezi kuwa na walimu wazuri na wakaweza kufundisha vizuri, lakini hatuwezi kuwa na wanafunzi ambao baadae tunategemea wawe wataalamu kila kitu tulichonacho sisi kinahitaji afya, tena afya bora. Mhe. Spika, katika hili nimuombe Mhe. Waziri kufanya upendeleo wa makusudi katika mgao wa zile fedha za wizara basi sekta ya afya waingiziwe fedha kama walizoziomba ili kuepukana na yale malalamiko ya wananchi, kwa sababu hii ni sekta inayowagusa wananchi moja kwa moja. Kwa hivyo, tukisema tunawaingizia fedha nusu na wakashindwa kutekeleza majukumu yao kila siku tutamkamata hapa Mhe. Waziri, tutamkamata Mhe. Naibu Waziri lakini *solution* ya hili pia ni kuingiziwa bajeti yote ambayo wameiomba, Mhe. Waziri naomba sana ulizingatie hilo.

Mhe. Spika, nije katika mwelekeo wa matumizi, katika mwelekeo wa matumizi kwenye kitabu ukurasa wa 32 imeelezwa kuwa matumizi ya mishahara yatakuwa ni bilioni 324. Lakini Mhe. Spika, nilikuwa nina suala kidogo Mhe. Waziri akija aje anipe ufafanuzi wake. Kuna walimu ambao wameajiriwa tokea mwezi wa nne mpaka huu mwezi wa sita tulionao walimu hawa hawajalipwa mishahara. Wanapokwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanaambiwa kwamba majina yao yameshapelekwa Wizara ya Fedha, lakini huku hakuna kinachopatikana. Lakini katika kundi hilo hilo wapo walioajiriwa na wameshalipwa miezi miwili, lakini ule mwezi mmoja wa nyuma hawajalipwa. Suala langu je kwa hawa ambao hawajalipwa mishahara yao itatokana na hizi bilioni 324 au ni katika bajeti iliyopita? Na hawa ambao wamelipwa miezi miwili mwezi mmoja hawajalipwa je watakuja kulipwa *arrears* yao kwa ule mwezi ambao haujabakia. Hapa nilikuwa naomba kupata ufafanuzi kwa sababu haya malalamiko yapo hawezi mtu kuajiriwa muda wa miezi mitatu ukasema mtu umemuajiri na hujamlipa mshahara, kwa kweli hali hii itakuwa si nzuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja utakuja kunipa ufafanuzi wa hili.

Mhe. Spika, sasa nije katika vipaumbele vya kitaifa, kifungu cha 61(c) kuimarisha miundombinu ya msingi ikiwemo barabara na nishati. Mhe. Spika, niipongeze sana serikali katika kuhakikisha inaimarisha miundombinu ya barabara lakini vile vile ya nishati. Mhe. Spika, katika hili mimi nitazungumzia nishati, kwenye eneo la nishati katika mpango mkuu wa serikali unaelekea kuwa na miundombinu mbadala ya nishati. Katika hili niiombe serikali kuharakisha mfumo huu ili kuwasaidia wananchi kiuchumi kwa sababu wataweza kupata umeme kwa bei nafuu katika kuendesha shughuli zao na wao wataweza kulipa kodi inayostahiki kwa wakati na hapo serikali itaweza kuinua uchumi wake. Kwa sababu eneo kubwa la uchumi wa nchi yetu huchangiwa na wananchi kwa kulipa kodi. Mheshimiwa niiombe serikali kuhakikisha kwamba hii nishati mbadala inafanywa haraka na inashuka kwa wananchi ili kupata unafuu wa maisha, lakini vile vile kuweza kuongeza pato la taifa.

Mhe. Spika, baada ya hayo nimpongeze tena Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa umakini wake na utekelezaji mzuri wa majukumu yake. Mwisho kwa niaba ya wanawake wote naunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwantatu naomba sasa nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Asha Abdalla Mussa ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kuchangia machache juu ya hotuba hii ya Bajeti ya Serikali. Kwa kuanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia bado tukiwa ni wazima wa afya na tukiendelea na mfungo mtukufu wa mwezi wa Ramadhani ikiwa leo ni mwezi 21, ningewaomba sana wananchi na nikawanasihi sana kumalizia mwezi huu mtukufu wa Ramadhani na kuweza kukabiliana na sikukuu ya *Eid el Fitri* kwa salama na amani bila ya kuwa na hofu au kufanya yale yote mabaya ambayo Mwenyezi Mungu anayachukia.

Mhe. Spika, kwa kuanza niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada yake kubwa inayoichukua kwa wananchi wake wa Zanzibar, lakini pia nizipongeze sana wizara zote ambazo zinaisimamia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuifanyia kazi na kuwatumikia wananchi wake kwa hali na mali.

Mhe. Spika, pia nimpongeze zaidi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jitihada yake kubwa anayoionesha katika kipindi hiki kifupi tangu kuwepo kwake mpaka muda huu tunaona matumaini makubwa yanakuja kwa wananchi wa Zanzibar na *inshaallah* Mwenyezi Mungu azidi kumpa moyo na nguvu na ari na uwezo wa kuyatenda yale yote yaliyo mema na kuyafichua yale yote yaliyo mabaya ili serikali yetu ya Zanzibar izidi kuongeza pato lake, na izidi kuongeza hali nzuri ya kiuchumi. Pia azidi kumpa moyo Mhe. Rais kwa kuzidi kuwaongeza wananchi wake mishahara ilimradi nchi yetu iendelee kwenye hali nzuri, lakini pia na wananchi wetu wazidi kunufaika na maisha mazuri ili waweze kuona manufaa ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, moja kwa moja nikianza katika mchango wangu huu niende kwenye vipaumbele vikuu vya kitaifa. Mhe. Spika, katika vipaumbele hivi vikuu vya kitaifa ningependa nizungumzie machache sana ambayo yameguswa zaidi kwenye hivi vipaumbele. Mhe. Spika, kwenye kipaumbele cha (d) kuendelea kuimarisha utalii hususan katika maeneo yaliyotajwa awali katika mpango wa matokeo ya ustawi. Mhe. Spika, kwa kweli tunafahamu kwamba suala la utalii

katika nchi yetu ni suala ambalo linaiongezea bajeti serikali yetu, lakini pia ni suala ambalo linawapa moyo wananchi wetu na kuweza kunufaika na kujikwamua katika hali ngumu ya kimaisha.

Mhe. Spika, utalii utatuongezea pato na unatupa moyo kwa kweli kwa wananchi wetu, lakini hasa kwa vijana wetu kuweza kujiajiri wao wenyewe, kwa sababu tunajua kwamba ajira ya serikali bado ni chache lakini serikali yetu inajitahidi kupambana juu ya hili ili wananchi wake waweze kunufaika na waweze kupata ajira na hata kuweza kujiajiri wao wenyewe. Kwa vile imeliona suala hili ndio ikaimarisha suala la utalii ili wananchi wetu na wao waweze kujihudumia wenyewe, waweze kupata maisha yao kwa vizuri.

Mhe. Spika, suala la utalii ni suala ambalo kwa kweli linatia unyonge kwa upande mwengine ukiliangalia, kwa sababu ni suala ambalo serikali yetu kama italiangalia kwa umakini zaidi ni suala ambalo linaweza likaweka pato kubwa la nchi yetu na bajeti ikazidi kuongezeka kutoka hiyo asilimia iliyopo ikaongezeka zaidi. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iliangalie suala hili kwa umakini zaidi na kwa macho mengi, kwa sababu tunajua kwamba walaji wamo wengi tangu ndani ya wizara lakini pia hata humo kwenye sekta na pia huko kwenye mahoteli lakini hata kwenye ngazi za chini, kuanzia kwenye Shehia mpaka kwenye Wilaya na Mikoa.

Mhe. Spika, suala la utalii linapita maeneo mengi, kwa kweli suala hili linaanzia kwenye Shehia, linakuja kwenye Wilaya, linakwenda kwenye Mkoa mpaka kumalizia taifa. Kwa hivyo, tunafahamu kwamba makusanyo haya yanapita sehemu nyingi, kwa vile makusanyo haya yanapita sehemu nyingi hayafikii lile lengo la serikali yetu kuweza kukusanya lile pato hasa linalotakiwa, hususan tukizingatia watalii hawa wanapokuja kwenye mahoteli yao wanakuwa tayari wameshafanya *booking* kwa hivyo kila mwenye hoteli anafahamu mimi kwa kipindi hiki ninaweza nikapokea wageni wangapi au ninaweza kupokea watalii wangapi.

Lakini sifikirii kwamba serikali inalifahamu hili kuwa kila hoteli imesha-*booking* wageni wangapi na wageni hawa watafikia hoteli gani na hoteli gani ili kuweza kukusanya yale mapato zaidi kwa uimara zaidi na serikali yetu ikaweza kuingiza pato basi kuna hali za kijificho jificho ambazo zinakuwa zinafanyika ili wale walaji wanapata yao humu humu na kupelekea wao wanapata posho kubwa zaidi. Hata ile serikali yetu ambayo ndio imeliweka suala hili ili iweze kusaidia na wananchi wake waweze kunufaika kwa kuongezewa masuala mengine ya mishahara lakini pia na kuimarisha masuala yetu mengine ya kiafya na ya kijamii. Kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie kwa umakini suala hili na alivalie njuga suala la makusanyo ya mapato kupitia kwa wawekezaji lakini pia kupitia kwa wageni ambao wanaingia ndani ya nchi yetu na kufikia ndani ya mahoteli.

Mhe. Spika, tunafahamu kwamba mahoteli yanakusanya pato kubwa sana na wao wanajiimarisha zaidi kuliko sisi wenyewe ambao tupo hapa ndani ya nchi. Kwa hivyo, tunaona manufaa zaidi yanakwenda kwao wao kuliko sisi ambao tupo hapa ndani ya nchi yetu na hatuwezi kunufaika na hili suala la utalii. Kwa hivyo, tunaona kwamba suala hili bado lina changamoto kubwa na walaji wapo wengi Mhe. Waziri. Walaji wa suala hili la utalii na ukusanyaji wa mapato bado wapo wengi. Kwa hivyo, nikuombe sana Mhe. Waziri suala hili kama ulivyoweza kuyafanikisha yale mengine na ukaweza kuyatumbua majipu yale mengine

basi na suala hili nalo uliwekee kipaumbele ili liweze kufatiliwa kwa makini zaidi na kwa utaratibu mzuri ambao unahusika, hususan ukishirikiana na hii idara yako ya *ZRB*, Mhe. Waziri ningekuomba sana suala hili uliangalie kwa umakini wake.

Mhe. Spika, nikiendelea pia zaidi katika vipaumbele hivi kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo za elimu na afya. Mhe. Spika, serikali yetu ya Zanzibar inajitahidi sana, sana, sana kuimarisha huduma hizi, tunamuona Mhe. Rais jinsi anavyohangaika au anavyopigana kuimarisha suala hili la elimu na afya katika nchi yetu. Tunafahamu kwamba nchi yetu hii ina visiwa viwili Unguja na Pemba, lakini kwa kweli suala hili la elimu na afya ni suala la kupewa kipaumbele zaidi kwa wananchi wetu, kwa sababu bila ya elimu huwezi ukafanya kitu na bila ya afya huwezi ukasoma. Kwa hivyo, kwa vile tunahitaji kutafuta elimu basi serikali ijitahidi ili tuweze kupata elimu, na elimu sio ya kwenda skuli tu au ya kusoma skuli na vyuo. Lakini kuna elimu nyingi ambazo zinapaswa kufahamika kwa wananchi hususan za ujasiriamali lakini pia na elimu za afya na mazingira.

Mhe. Spika, elimu ya afya na mazingira kwa kweli sasa hivi serikali yetu ijitahidi kutoa elimu hii ili wananchi wetu waweze kuwa nayo elimu hii, kwa sababu tunaona kwamba suala la miripuko ya maradhi kwa sasa hivi kila siku yanaongezeka hujui kipindi cha masika wala cha vuli, wala hujui kipindi cha kipupwe, ilimradi maradhi kila siku yanaibuka. Lakini ukizingatia pia uimarishwaji wa mazingira katika nchi yetu sasa hivi umekuwa ni mbovu. Kwanza (a) kutokana na zile tamaduni ambazo zilikuwepo kipindi hicho na sasa hivi imekuwa ni tofauti, tamaduni za kusafisha mazingira kwanza mtu binafsi yake yeye mwenyewe ndani ya nyumba yake iliyomzunguka na nje basi tunaona kwamba ni tofauti. Kwa hivyo, serikali ichukue jitihada kubwa ya kuwausia wananchi juu ya suala hili la mazingira lakini na kujali afya zetu wenyewe, elimu zitolewe kwa kila hali kupitia sekta zote lakini pia kupitia mashirika yote na wizara zote, kwa sababu kila wizara ina mwananchi na kila wizara inahusika na jamii. Kwa hivyo, hili suala la elimu serikali iliangalie kwa kipaumbele zaidi juu ya elimu ya afya na mazingira yaliyotuzunguka.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye suala la uimarishwaji wa kilimo, uvuvi na maji. Mhe. Spika, mimi nitazungumzia zaidi suala la Kilimo. Tunamuona sana Rais wetu wa Zanzibar jinsi anavyopambana na suala la umasikini katika nchi yetu, ukweli ni kwamba umasikini katika nchi yetu hauwezi kuondoka kama hatutoliimarisha suala la kilimo. Suala la kilimo katika nchi yetu ndio uti wa mgongo wa maisha yetu kutokana na mazingira tuliyonayo, lakini pia kutokana na asili tuliyotokana nayo. Kilimo tunaona kwamba ndio uti wa mgongo wa maisha yetu, serikali iliangalie sana suala la uimarishwaji wa kilimo ili kuweza kuwanufaisha wananchi wake lakini pia kuweza kuongeza pato la serikali yetu.

Mhe. Spika, sasa hivi kilimo kinawekwa kwenye kila miundombinu, yaani kinapewa kila hadhi ili kiweze kuwa imara na kiweze kunufaisha wananchi. Lakini tunaona kwamba bado serikali haijakaa hasa ikaliangalia kwa umakini zaidi suala hili la uimarishwaji wa kilimo. Kwa sababu tunapiga kelele sekta ya kilimo iimarishwe kwenye mambo ya umwagiliaji, sijui mambo ya pembejeo, mambo ya kuletwa matrekta, lakini bado tunaona serikali juu ya suala hili haijalitilia mkazo na haijalipa kipaumbele. Kwa sababu unapofika wakati wa makulima tunafahamu kwamba kila kilimo kina msimu wake, tukija kwenye mpunga una msimu wake, lakini tukija kwenye mazao ya matunda na mengineyo pia yana misimu yake. Kwa hivyo, serikali iweze

kujipanga juu ya suala hili na iifahamu hii miongo ya hivi vilimo vinavyohusika katika hii nchi yetu.

Kwa sababu kilimo cha mpunga tunafahamu kwamba kina misimu zaidi ya mitatu, lakini mazao nayo pia yana misimu mkubwa na mdogo. Kwa hivyo, tungeiomba sana serikali ikaijua hii miongo lakini ikajua na hizi taratibu za kilimo jinsi gani wakulima wanapambana kupigana katika kulima mazao haya na kulima vyakula mbali mbali ili nchi yetu ikaweza kuendelea vizuri na hali ya kiuchumi ikazidi kukua na wananchi wetu wakaondokana na ile changamoto ya dhiki ya maisha, wakiwa wanalima kila kitu wao wenyewe na wakaweza kujinunulia wenyewe nina hakika hapa hata masoko yetu yatakua na serikali itazidi kuongeza pato la serikali yake na wananchi wakaweza kunufaika.

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri juu ya suala la kilimo, tumeona kwenye bajeti yake mapesa yamo mengi yaliyopelekwa kwenye bajeti hii ya kilimo kwa mwaka wa fedha huu wa 2017/2018, lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri akasimamia kwa umakini zaidi juu ya sekta hizi na wizara hizi zote alizozipa mapesa haya, akahakikisha hawa watendaji wote wanaifanya hii kazi ya kusimamia pesa hizi na kuzifanyia kazi. Kwa sababu tunapiga kelele hapa kwamba ziingizwe kwa wakati, nina hakika Mhe. Waziri kutokana na upeo wake alionao pesa hizi ataziingiza kwa wakati na tunamuomba kazi ifanyike ili serikali yetu na wananchi wetu waache malalamiko, waache kuisakama serikali yetu kwa sababu ya watu fulani, kwa sababu ya watu baadhi ambao wanarejesha nyuma maendeleo ya nchi yetu, ambao wanarejesha nyuma maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu hii lakini pia kilimo hiki hiki ndicho kitakachosababisha masoko kukua ndani ya nchi hii. Pia kilimo hiki ndicho kitachosababisha wananchi wetu waweze kuwa mstari wa mbele kuipigania serikali yao, lakini pia kuitumikia kwa hali na mali endapo wataimarishwa kwenye sekta ya kilimo. Kwa sababu kila mtu nina uhakika anaweza kulima, anayekaa mjini, anayekaa shamba, anayekaa kwengineko, kila mtu uwezo wa kulima anao na akipewa elimu basi anaweza kufanya makubwa zaidi juu ya nchi hii na nchi yetu tukaiona kwamba iko juu kimapato, iko juu kiasilimia, iko juu katika utendaji. *(Makofi)*

Mhe. Waziri ningemuomba sana akalisimamia suala hili akawasimamia watendaji wote. Mhe. Waziri asiwaogope, asiwaonee haya, asiwatizame machoni kwa kuona huyu ni ndugu yangu, huyu ni nani, yeye mtumbue anayekaa vibaya amuondoe ili serikali yetu iweze kuleta manufaa ya wananchi wake na wananchi wetu waweze kunufaika na nchi yao hii na maendeleo yaliyomo ambayo tunayasababisha sisi tuliokuwemo humu ndani ya Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo machache na mimi niseme naiunga mkono hotuba hii ya serikali endapo itasimamiwa kwa umakini zaidi, kwa huo mstari wa mbele ninaouona huko na watu hao waliokuwepo hapo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame kwa mchango wako, anayefuata sasa ni Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa fursa hii kutoa mchango wangu katika hotuba hii. Lakini awali ya yote na mimi nasema namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwenye kurehemu, aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote.

Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nasema kwamba leo nimefiliwa na Katibu wangu wa Jimbo la Chake Chake Ndugu Juma Omar ambaye amefariki pale Chake Chake jana jioni na leo anazikwa. Kwa hivyo naomba tumtakie kheri aende safari ya salama.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi nataka kwanza nimshukuru sana, nimuombee dua sana Mhe. Rais kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya na kwa nia ya dhati ambayo kwa kweli ni kiongozi mmoja ambaye Mwenyezi Mungu ametuletea kama ni kiongozi wa hidaya ambaye amekuja kutuokolea nchi yetu katika mazingira. Kwa sababu mtu huyu roho yake Mwenyezi Mungu kamjaalia haina tamaa kubwa, ni kiongozi ambaye anapenda wananchi wake, ni kiongozi ambaye anapenda nchi yake na kiongozi ambaye anapenda maendeleo. Kwa hivyo, hatuna budi lazima tuweze kumsifu kwa sababu ya uendelezaji wake mzuri na ni mifano ya nchi nyengine ambayo hata Mhe. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano huwa anamsifia sana Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uungwana wake.

Mhe. Spika, na mimi katika kuchangia nataka kusema kwamba ahadi za Mhe. Rais ni kiongozi pekee mpaka muda huu, ni mtu ambaye ametoa ahadi na ahadi zake anazitekeleza kwa vitendo. Kwa hivyo, niweze kusema tu kwamba amejitahidi katika zile ahadi zake mojawapo ilikuwa ni kutwambia kwamba atatupandishia mishahara ya kima cha chini kwa asilimia mia moja, watu wengi wakawa wanasema hii ni ndoto wala haiwezekani. Lakini nataka niwahakikishie Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote kwamba hii leo ni mashahidi wananchi wote, wafanyakazi wote magego yote yako nje na wameamini kile alichokisema, kwamba mishahara yote ametimiza ile ahadi yake.

Mhe. Spika, chengine ni kwamba Mhe. Rais amejitahidi katika kusimamia bajeti, amejitahidi katika kusimamia maendeleo na mpaka sasa hivi anajitahidi kwamba kwa asilimia 65 tunajiweza katika kujiendeleza bila ya kutegemea wahisani. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo Mhe. Rais ameweza kulitekeleza.

Mhe. Spika, haya ni mafanikio ukipata kiongozi ambaye atakuongoza na tukafika katika malengo huyu mtu habahatishi ni mtu ambaye naweza kusema alijipanga na kwa kweli maneno yake na vitendo vyake vinakwenda sambamba. Kwa hivyo, nataka niwaambie wananchi kwamba tumuunge mkono Dkt. Ali Mohamed Shein na yale maendeleo ambayo anayaleta basi tuyaunge mkono kwa wale waliokuwa wana nia ya kuyaharibu wasiyaharibu, maana yake hata mbele ya Mwenyezi Mungu watakuja kujibu. Wasione tu kwamba kuna tamaa ambayo inaweza akaona kama kuna tangi la maji ukalitoboa unamkomoa Dkt. Ali Mohamed Shein au unakomoa watu wengine, hukomoi lakini ni kujipalia makaa mwenyewe kama pweza, sijui baadae ukiwa katika umri ambao sasa unaomba maghufira utakuja kumuomba nani na Dkt. Ali Mohamed Shein atakuwa keshaondoka madarakani, sasa na yeye ndiye uliyemkosea zaidi kwa kuleta maendeoeo na wewe ukalitoboa tangi la maji.

Kwa kweli nilikuwa niwasihi wenzangu ambao wanafanyiwa maendeleo halafu wao wanayarudisha maendeleo nyuma. Kwa hivyo, ningeomba sana maendeleo yanapokuja ni

gharama kubwa sana, maendeleo yanapokuja kuna vitu vimenyimwa katika sehemu nyengine mkaletewa nyinyi, halafu kama hamkuvitunza pale hamumkomoi mtu mnajikomoa wenyewe lakini pia yule mtu ambaye anafanya madhambi yale Mwenyezi Mungu hamsamehe.

Mhe. Spika, katika mambo ambayo naweza kusema kwamba katika mafanikio ambayo tumefanikiwa ni mambo ambayo ni makubwa. Dokta Ali Mohamed Shein kajenga Hospitali ya Mkoani hakuna mtu aliyeamini kwamba hospitali ile itajengwa na Mkoani ile itabadilika kwa kipindi kile kile alichosema. Nataka tuseme waliokuwa hawajenda Pemba na waende wakaangalie Mkoani, huwezi kuijua kama hospitali ile imeteremshwa Mkoani maana yake naweza kusema katika Tanzania hii basi labda ni ya kwanza. Sasa naomba tena Wizara ya Afya, naomba tena wananchi wa Mkoani waitunze sana hospitali ile kwa sababu si rahisi kujengwa tena hospitali kama ile kutokana na hadhi yake iliyonayo ni pesa nyingi sana zimepotea. Kwa hivyo, madaktari lengo lile ambalo limejengewa kwa kunufaisha wananchi wake wa Mkoani na wananchi wengine ambao watakwenda kupata matibabu pale, kwa takriban wananchi wote wa Pemba na wengine Watanzania wawatibu vizuri kwa lengo lile lile alilokusudia Dkt. Ali Mohamed Shein. Kwa hivyo, ningeomba sana.

Mhe. Spika, lakini pia nataka niseme tulizungumza suala la barabara ya Fuoni tukaambiwa milenium hapa sijui watu wote, lakini Dkt. Ali Mohamed Shein amejenga barabara ile kwa kipindi cha miezi mitatu hakuna mtu aliyeamini. Nataka niseme leo yale mazogo yote ya wawakilishi waliokuwa wakisema habari ya vumbi katika barabara ya Fuoni wameyasahau na wameona nini ambacho Rais wetu aliwaambia na ametekeleza. Kwa hivyo, nawaomba kwamba Rais anapozungumza kuwa nitafanya mimi Dkt. Ali Mohamed Shein namchukulia dhamana atakachokisema kwamba nitafanya yule hakurupuki wala habahatishi; ninachowaambia ameshasema atafanya Darajani *corridor* nataka wananchi, nataka wawakilishi tumpe ushirikiano Mhe. Rais na ninawahakikishia Darajani *corridor* itajengwa. Nachukua dhamana hii mimi mwenyewe kutokana na upeo wa Dkt. Ali Mohamed Shein jinsi ambavyo maendeleo yake yanakuwa, sichukulii kama Waziri wa Fedha lakini namsifia Rais wangu kutokana na vitendo ambavyo alishavionesha, amesema atafanya ng'ambo tuitakayo nawahakikishia kwamba ng'ambo tuitakayo itakuja, zaidi ni ushirikiano tu, tumpe ushirikiano.

Sasa hivi Chake Chake waliokuwa hawajenda kwa muda wa mwaka mmoja na wende wakaiangalie Chake Chake jinsi maendeleo yake yalivyo, nina uhakika kwamba baada ya miaka mitano Chake Chake itabadilika. Kwa hivyo, ninachowaomba nchi nzima kwa takriban ni kutoa maendeleo, kutoa ushirikiano kwa kumpa Rais ushirikiano wa nguvu kutokana na mwenyewe alivyokuwa amejipanga ili kuiletea maendeleo.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpe ushauri Mhe. Waziri kutokana na maendeleo ambayo tunayapata, ziko hizi E za mambo ya elimu, E mambo ya afya, E zipo nyingi hizi ambazo zinatokana na *E-Government* ambazo wananchi wengine hawajajua mategemeo ambayo yatakuja. Lakini mimi ningezungumza sana Mhe. Waziri kwa ushauri wangu akaweza kuiangalia hii habari ya manunuzi ambayo kwa kweli ni kitu ambacho kinatupa vikwazo au kinatukwaza kutokana na mambo ambayo labda niseme yataweza kutusaidia asilimia 75 ya pesa za serikali zinakwenda katika mambo ya manunuzi. Manunuzi ndio yanayotumaliza, manunuzi ndio yanayotuongoza, manunuzi ndio kila kitu kinapoanza.

Sasa mimi ningetoa manunuzi yakipatikana katika manunuzi yetu ambayo tumeyapanga kwenye E nawahakikishia kwamba tuta-*save* zaidi ya asilimia 35, ambapo ndio pesa ambazo tunazisubiri kutoka kwa wahisahi, zile zitapata fungu la kuingia pale kama wanavyosema viongozi wetu pesa za wahisani tunazitaka lakini hatuzitaki kwa masharti magumu, tunazitaka kama ni washirika wetu, kama ni wenzetu, tunazihitaji lakini isiwe tena kila pakitokea uchaguzi kwanza kuzuwiwe, Tanzania ni moja ya nchi ambayo inafanya uchaguzi katika demokrasia ya hali ya juu sana, ni moja ya nchi ambazo zinafanikiwa sana katika kuendeleza uchaguzi wake, lakini kila mmoja katika mataifa makubwa yana *interest* zake na mambo yao. Sasa kama kuna nchi ambazo *interest* zake zinakuwa kwamba ni mpaka tuwekewe vikwazo mimi nigeshauri tukiweka hili suala la manunuzi pesa yetu ambayo ni asilimia 75 inapotea hapa basi itapunguza mambo mengi.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi ambayo kwenye manunuzi yanatokezea, kuna gharama za *tender*, kuna ununuzi wa wakati, kuna mambo ambayo pesa zetu hazipotei ovyo, kuna rushwa na mambo mengi. Mimi ningemshauri waziri hii akiichukua vizuri katika mambo ya mtandao, akatuweka vizuri kwenye sekta za afya. Sasa hivi unaweza ukazungumza na daktari hata kama yuko pahali gani akakupa matibabu yako ukaendelea nayo. Kwenye sekta za elimu unaweza ukazungumza na *lecturer* aliyepo popote akakusaidia, lakini sasa na upande wa manunuzi tukiweza kwenda vizuri basi na manunuzi asilimia nyingi tutakuwa tumepona badala ya hii mikataba mibovu, mambo mabovu yote haya yataondoka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili ningemuomba sana Mwenyezi Mungu akimjaalia kumpa nguvu basi tuweze kwenda na hili litatusaidia sana.

Lakini Mheshimiwa mimi nataka nizungumzie jengine ni kwamba ahadi ambazo tumezitoa kwenye mawizara yote Bajeti ambayo tumeizungumzia kwenye mawizara yote, tumeizungumzia sana kwamba ni matumaini yetu kwamba tutafika lengo la lile tulilokusudia. Mhe. Spika, mara nyingi tunakwama kutokana na bajeti ambayo hatufikii hapa tumeshajilabu sana kutokana na kila wizara kwamba itafanya hivi itafanya vile na matumaini ya wananchi huko tayari tushajua kama barabara yangu ya msingi itajengwa kesho kutwa kuna barabara nyengine zitajengwa, waliokuwa hawapati maji watapata. Lakini kama bajeti itakuwa haifikii lengo basi mara nyingi tunakwama njiani. Sasa ningemuomba waziri katika jitihada zake hizi hizi na mimi namuamini sana akatekeleza ahadi zake na maneno yake kama yalivyokuwa ili kutafikia malengo ambayo yatakuwa.

Lakini pia kila wizara ilikuja na changamoto sasa ningeomba wananchi, ningeomba Waheshimiwa Wawakilishi tuisaidie serikali katika kodi ikipata kodi zaidi na kodi zenyewe za halali mafanikio mengi ambayo yatapatikana ni pesa. Sasa kama sisi tunataka kutengenezewa nchi yetu majimbo yetu na wananchi wetu basi tusichoke kuwafahamisha wananchi wetu kwamba kodi ndio serikali ambayo inasaidia kufanya mambo mengine.

Kwa hivyo, sifikirii kwamba kuna watu wengine viongozi ambao wanamwambia mtu usilipe kodi sijui alikusudia nini katika kuwaendeleza wananchi maana yake bila ya kodi hatutokwenda popote serikali inaendeshwa na kodi. Kwa hivyo, ningeomba sana wale viongozi ambao wakati mwengine wanakuwa kama kutia ushawishi ambao sio ningeomba na suala hili wakaachana nalo. Kodi ni kitu muhimu bila ya kodi wanafunzi hawatosoma wala hatutofanya kazi wala hatutofanya kitu chochote, hatutojenga barabara, hatutofanya kitu chochote. Ningeomba sana

wale wanasiasa ambao hawana la kusema wakanyamaza wakamuachia Dr. Ali Mohammed Shein aendeleze Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nilikuwa nazungumza sana kuhusu suala la ardhi. Dr. Ali Mohammed Shein amelipatia ufumbuzi wa kutosha, Dr. Ali Mohammed Shein ni mtu ambaye kusema kweli katika mazingira ambayo kipindi cha miaka hii ambayo mitano kwa sita aliyoingia madarakani serikali imerudi sana katika neno lile tunalolizungumza kwamba ardhi ni mali ya serikali. Amekubali kuizungumzia kwamba ardhi ni mali ya serikali tokea enzi hizo ambazo baada ya Mapinduzi ilikuwa na lengo la kuzungumza kwamba ardhi ni mali ya serikali. Tumejisahau tumepoteza mambo mengi.

Lakini kitu cha msingi zaidi hata sheria ambazo zilitungwa pia tumezisahau wananchi wamekuwa wanajiendeshea wanavyotaka wenyewe serikali nayo ilikuwakubalia kufanya kila kitu. Lakini sasa hivi ni wajibu wetu wa kuzirudisha sheria zile zile ambazo tumezitunga ili tukaisimamia serikali katika ardhi na mambo yetu. Maneno mengi Mheshimiwa wakati wa Bajeti ya Ardhi yalikuja watu wanaotoka nje wengine hawa nia njema lakini zaidi ni kuja kuchukuwa pesa kwa sababu ardhi sisi tulikuwa hatuijui faida yake, tunakaa tunafanya kila tunachokiona, kila mtu anafanya anavyotaka.

Lakini nimuombe tena Mhe. Waziri nguvu za Wizara ya Ardhi aziongeze zaidi ili ardhi irudi kwenye mali ya serikli vile vile na irudi kwenye wananchi vile vile. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili akalichukua katika uzuri wa uhalisia.

Lakini nataka pia Waziri alitizame suala la maji, uhai wa maji watu wengi wameshasema bila ya maji hakuna uhai, suala la maji waziri aliangalie vizuri Wizara ya Maji ijitahidi kujikita katika kuwapa wananchi maendeleo kwa sababu bila ya maji hakuna uhai. Ningeomba hilo vile vile likatizamwa lakini narudi tena na Wizara ya Elimu ina jukumu kubwa sana na ina matatizo makubwa sana bado shule ambazo zinakuwa za serikali zinakuwa kama ni shule ambazo tunazungumza kama watoto wetu tunakwenda kuwatupa hatuwasomeshi, wakati sio lengo la serikali ni neno ambalo tunalizungumza elimu bure ni kwamba mtu asilipe pesa sio kwamba asisomeshwe.

Sasa ningeomba waziri ukalitilia mkazo na kama kuna pesa ambazo zinahitajika kwenye Wizara ya Elimu kuna mawizara ambayo Mhe. Waziri ukafumbia macho ukamwambia subiri lakini Wizara ya Afya, Elimu, Maji hizi lazima tuzipe kipaumbele katika mazingira mazuri sana.

Lakini pia nikupongeze sana Mhe. Rais lakini kwa kupitia Mhe. Waziri vile vile matumizi mazuri ambayo kidogo katika mambo ambayo pesa tukishakutuliwa lile si shamba la bibi Mhe. Waziri fuatilia pesa zako lile si shamba la bibi pesa akishepewa muhasibu akishapewa nani ukaambiwa zishaingia sio zimeshaingia wewe unajua umehangaika sana Mhe. Rais amehangaika sana wananchi wamehangaika sana katika kutoa kodi zao, isiwe tena zimeshaingia zililetwa zitumikie wananchi kwa nia njema.

Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri ushazichuma lakini na kuzitumia zifuatalie kwa sababu zinakuwa kama vile wewe umetia maji kwenye pakacha unayatia yanavuja haiwezekani Rais anahangaika anaomba misada halafu unatia maji kwenye pakacha haiwezekani. Lazima hili nalo

ulifatilie vya kutosha kwa sababu ndio kile kimeshapatikana lakini kinaondoka bila ya mahesabu.

Kwa hivyo, Mheshimiwa malengo mazuri hatuwezi kufanya jambo lolote kwa wakati huu tulionao bila ya pesa, lakini tunapoitapa pesa ile basi tuithamini sana kwa sababu malengo yaliyokusudiwa tuyafikie. Hii itatupa muelekeo na maneno tunayoyasema yatakuwa yanatekelezeka kwa sababu lile tulilolisema kama tunavyosoma bajeti yetu tunachokipata tunatumia pale pale ni kwamba tumeshajikita kwenye hapa. Katika Bajeti inayokuta haya yaliyofanyika mara hii yanandoka yanakuwa mengine, sio tunayarudia yale kwa yale na pesa zile ukiziuliza unaambiwa subiri *CAG* subiri kitu gani, sisi hatuna haja ya *CAG* kupita kupita kiasi *CAG* anaweka mahesabu kwamba tulitumia vipi na tukaweka vipi. Lakini malengo na matumizi ambayo ....

Mhe. Spika: Una dakika moja Mhehsimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mheshimiwa namalizia tu nakushukuru sana Mheshimiwa na leo Ijumaa nakuheshimu sana na kanzu uliyovaa leo Mhe. Spika, hongera sana.

Sasa nataka niseme la mwisho ni kwamba sisi ni Wawakilishi wa majimbo yote ambayo kwa takribani Chake Chake ndio mimi lakini na wenzangu tuliokuwa kwenye mazingira makubwa sana.

Mhe. Spika, ningeomba sana Wawakilishi wote najua ni wataalamu sana wa mambo ya siasa lakini tusikereke wala tusichukiwe na maendeleo au kuvunjwa kwa maendeleo au kwa matusi ya wananchi. Sisi tufanye kazi tuliotumwa na Chama cha Mapinduzi usiseme mimi kila nilifanyalo watu wanaliharibu wewe fanya watu wataona, wewe fanya waliokuwa na maendeleo watakushika mkono, wewe fanya Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako namwita sasa Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Khadija Omar Kibano ajiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, kwanza nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika tukiwa hai katika kikao hichi cha bajeti cha mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watendaji wake wote wa wizara ya Fedha kwa kuhakikisha kwamba Mapato na Matumizi yaliyopatikana katika mwaka wa fedha wa 2016/17 yamekusanywa vizuri lakini pia wameweza kutumika ipasavyo.

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukurani zangu hizo niseme pia niwashukuru sana wale wote ambao wanahusika na ukusanyaji wa mapato na kuweza kufikia trilioni 1.08 ambazo sawa na ongezeko la asilimia 23 ya mwaka wa bajeti ya 2016/17.

Mhe. Spika, bajeti iliyopita ya mwaka 2016 tumeona utekelezaji wake lakini pia tuwapongeze sana kwa juhudi walizozichukua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo mwenyewe Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein lakini pia na Mawiziri wote ambao wapo.

Mhe. Spika, niseme kwamba pindipo makusanyo haya yatafikia asilimia mia moja ya lengo tulilojiwekea basi naamini kwamba vipaumbele hivi vya kitaifa ambavyo vimewekwa hapa vitatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Mhe. Spika, katika vipaumbele vya kitaifa vya mwaka 2017/18 kuna mambo mengi hapa yameelezewa. Lakini mimi kwanza nianze katika kuimarisha huduma za kijamii.

Mhe. Spika, nianze kwenye suala zima la Elimu. Mhe. Spika, kwa kweli tumpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kujali sana kabisa suala zima la elimu. Lakini pia niseme kwamba kwa mwaka huu wa fedha wametenga fedha kwa ajili ya kukamilisha madarasa 285 kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wote wanapata kusoma vizuri. Mhe. Spika, niseme kwamba fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha madarasa haya basi tuhakikishiwe kwamba Mhe. Waziri anawaingizia kwa wakati ili tuone kwamba wanafunzi wetu wanafaulu vizuri mitihani yao lakini pia wanapata hifadhi nzuri.

Mhe. Spika, nije katika suala zima la Afya, Mhe. Spika, sote tunafahamu mtu ni afya na tunafahamu kwamba tuna vituo vyetu vya afya vidogo vidgo lakini tunavyo vya Mikoa na pia tunayo Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, naamini kwamba fungu lililotengwa hapa katika kuimarisha huduma ya afya basi tutahakikisha kwamba likitumiwa vizuri huduma ya afya wananchi wetu watapata ipasavyo. Lakini hapa nilitaka kushauri serikali kwamba Mhe. Spika, tuone kwamba tuna mashine zetu hapo Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiweno *CT- Scan*, *X-ray*, *Ultra sound* na nyenginezo, lakini wananchi wetu wanapokwenda katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na wanajua kwamba hospitali ile ndio kimbilio la wanyonge kwa kweli wanakwenda wananarudi lakini huduma hizi hawazipati.

Naiomba sana serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanyia matengenezo mashine zote ambazo ziko katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuhakikisha kwamba tunapata wataalamu. Mhe. Spika, katika kitabu chake cha Bajeti Mhe. Waziri wa Fedha kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kukuza uwezo wa wataalamu wa afya. Mhe. Spika, suala hili mimi nalitilia mkazo hizi pesa zilizotengwa bilioni 6.09 basi zitumike kama ilivyokusudiwa kwa sababu utakuta katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja mgonjwa atakwenda pale lakini anapofanyiwa uchunguzi anaambiwa vyengine. Lakini akitoka hapo akienda hospitali nyengine za nje anaambiwa hana kitu. Kwa kweli sasa tuhakikishe kwamba fedha hizi ambazo zitakapopatikana wataalamu wetu wanasomeshwa ipasavyo na tuhakikishe kwamba tunakuwa na wataalamu wa kutosha katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, niende kwenye suala zima la maji, Mhe. Spika, tunafahamu kwamba hapa Zanzibar tuna tatizo kubwa la maji na kwa mwaka wa fedha huu tumeambiwa kwamba katika vipaumbele

ni suala la maji vitaendelezwa visima 26 zilivyochimbwa na Ras el Khaimah. Mhe. Spika, naomba sana serikali iangalie kwa jicho la huruma suala hili la maji kwa sababu wananchi wetu wanapata tabu sana kwa ajili ya maji na wanaoumia sana ni wanawake, mwanamke ana kazi ngumu ya kutafauta maji popote yalipo na bila ya maji hatuwezi tukala, bila ya maji hatuwezi tukakoga, bila ya maji hatuwezi tukafua.

Mhe. Spika, naomba sana serikali itizame kwa jicho la huruma suala la maji hili kwa Zanzibar liwe mwisho. Mhe. Spika, lakini pia niseme suala zima la ukusanyaji wa mapato bajeti tumeipanga lakini bila ya fedha hatuwezi tukatumia. Mhe. Spika, nimtake Mhe. Waziri wa Fedha ahakikishe kwamba kila panapo makusanyo yoyote ihakikishe mapato yale yanapatikana na uandaliwe utaratibu kama ulivyopangwa hapa kwamba zinunuliwe mashine kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato, kwani sasa hivi kila panapokusanywa mapato mengine yanaingia mfukoni huo mfuko wa serikali lakini mengine yanaingia kwenye mfuko binafsi.

Mhe. Spika, niseme kwamba hawa wafanyabiashara wetu wanahimizwa sana wanapofanya biashara zao watumie sana suala la risiti, tunaona kwamba tunapokwenda kutia mafuta kwenye sheli zetu tunapokwenda kwenye maduka makubwa lakini pia na madogo, wenzetu Tanzania Bara mfumo huu wa kutoa risiti kwa kweli unatumika ipasavyo.

Naomba sana serikali ihakikishe kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 basi Wazanzibari wote waweze kutumia risiti na wanapokwenda kununua bidhaa basi waweze kudai risiti, kwani tuone kwamba tukifanya hivi tutajua kwamba ule mfuko wetu wa miundombinu ambao unakusanywa kwenye suala zima la mafuta pamoja na umeme basi tuone kwamba zile fedha zinazopatikana pale basi zinaingia serikalini.

Mhe. Spika, niseme kwamba tumpongeze pia Mhe. Waziri wetu wa Fedha kwa kuamua kwa makusudi na kuwasikiliza Wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na kilio kikubwa cha ongezeko la pencheni ya wazee wetu ambao wastaafu. Katika kitabu chake tuona hapa shilingi bilioni 10 zimetengwa kwa ajili ya kuwaongezea pencheni wazee wetu. Hili kwa kweli tumpongeze sana na Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuliona suala hili na wao wazee wanaona kwamba serikali iko pamoja nao na pia wanapata imani kubwa katika kutumikia nchi yao.

Mhe. Spika, mimi kwa leo sina mengi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti mengi tumeyahoji kwenye kamati yetu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa na sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatia na Mhe. Khadija Omar Kibano na Mhe. Machano Othman Said ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shauri Moyo kuweza kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Mhe. Waziri ya Mapitio ya hali ya Uchumi pamoja na Mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kweli Mhe. Waziri wa Fedha katika kipindi kifupi baada ya kupewa dhamana hii ameonesha upeo

mkubwa, ameonesha maarifa makubwa na ameonesha uwezo mkubwa sana wa kuweza kusimamia Mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuhakikisha kwamba mapato hayo yanakwenda moja kwa moja kuboresha hali za maisha ya wananchi wetu. Namuombea Mungu Mwenyezi Mungu amjaalie awe na moyo huo huo na jitihada hiyo hiyo wala hizi sifa tunazompa hapa zisije zikamvimbisha kichwa baadae akaja akasahau haya ambayo tuliomwambia leo.

Mhe. Spika kwa mara ya kwanza ndani ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaanza kutaja *figure* inayoitwa *trilion* moja. Mhe. Spika, tulisema sana huko nyuma kwamba Zanzibar tukiweza kukaa vizuri, tukitulia vizuri nchi ikiwa haina matatizo hasa ya kisasa basi uchumi wa Zanzibar kukua una asilimia zaidi ya mia moja na hivi sasa katika hichi kipindi kifupi kwa kweli chini ya uongozi mahiri wa jemedari wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kweli yale ambayo tulikuwa tunayaota hivi sasa tumeanza kuyaona.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba haya mapato ambayo tunajivunia tuliyoyapata kwa kuvuka malengo yetu ya ukusanyaji *TRA, ZRB* pamoja na mapato ya serikali,bado kuna maeneo kama tutaweza kufunga msuli, basi tuna uwezo wa kuongeza mapato zaidi ya haya ambayo tuliyoyapata. Katika bajeti ya mwanzo niliwahi kumwambia hapa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, nikamwambia mheshimiwa sisi tutakushauri mambo mengi, tutakuonesha matundu mengi, kama utaweza kuyasimamia vizuri basi bajeti yetu itakwenda vizuri. Sasa haya ndio matunda yake na bado tutaendelea kumuonesha maeneo mengine ambayo tukijitahidi basi tuna uwezo wa kuweza kuongeza mapato, na kwa sababu bajeti kuu ya serikali ni mambo mawili tu, ni *revenue* na *expenditure* ni makusanyo na matumizi. Tukiweza kukusanya zaidi, tutaweza kutumia zaidi na tutaweza kuboresha maisha ya watu wetu.

Mhe. Spika, kabla sijaenda kwenye kabla sijaenda kwenye uchambuzi wangu wa moja kwa moja nataka nieleze matumaini. Mimi juzi nilisema hii sio bajeti ya mageuzi, lakini hii ni bajeti ya matumaini kwa wananchi wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika ku-*peruse* hivi vitabu viwili vya Mhe. Waziri nilijaribu ku-*peruse* ukurasa wa 36 wa kitabu chake ambacho chenye mapendekezo ya bajeti yetu ya mwaka huu wa 2017/2018, hasa katika ule ukurasa wa 36 kifungu cha 77 kinachoeleza, mazingatio maalum ambayo serikali yetu imeyapa kipaumbele.

Kwa mfano, Mhe. Spika, ukiangalia deni la *TANESCO* ilikuwa ni mzigo wa mwizi, maana yake mzigo wa mwizi Mhe. Spika, mwizi anaweza akabeba mzigo anakwenda nao mbio, lakini ukimkamata tu akiuweka chini ukimwambia aubebe hauwezi. Sasa hili ndio lilikuwa deni la *TANESCO*. Deni la *TANESCO* lilizungumzwa sana kwa miaka mingi, watu wakaanza kukoseana na wakakosa imani. Lakini tunamshukuru sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati akiwa safarini baada ya kurudi tu uwanja wa ndege, waandishi wa habari walimchokoza wakamwambia sasa mzee unasemaje maana yake umeme utakatwa. Akawaambia tutawasha vibatari. Kwa hivyo, wananchi wengi walishtuka Mtume! umeme utakatwa tutawasha vibatari hali itakuwa vipi.

Mhe. Spika, kumbe Rais wetu sio mtu wa papara alikaa akatafakari akauliza kwani nini tatizo. Tatizo akaambiwa tunadaiwa bilioni 120 za deni la umeme. Akawaagiza watu wake *ZECO* akawaambia nendeni kakaeni na wenzenu wa *TANESCO* muangalie deni halisi tunalodaiwa, sio

deni la kubambikizwa, kakaeni muangalie deni halisi tunalodaiwa halafu hilo deni tunalodaiwa sisi tutakubali kulilipa.

Mhe. Spika, nataka tena nimpongeze tena Mhe. Rais, lakini vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, kwa sababu agizo lile la Mhe. Rais Mhe. Waziri alilifanyia kazi. Kwa bahati nzuri na mimi alinishirikisha katika baadhi ya vikao vyao vilivyofanyika Tanzania Bara, baina ya *ZECO* na *TANESCO*. Katika mjadala ule deni lilikuwa bilioni 120, matokezeo yake *ZECO* wakasema deni tunalodaiwa sisi ni bilioni 65, tukajenga hoja mpaka imefika pahala deni lile ambalo lilikuwa linaambiwa bilioni 120, matokezeo yake kumbe deni halisi tunalodaiwa ni bilioni 65, kwa kweli hiyo kwanza ni kazi moja kubwa.

Lakini kazi nyengine ya pili iliyofanywa na serikali hii Mhe. Spika, ni kuangalia namna gani ya kulimaliza deni lile, deni lililokaa zaidi ya miaka 15 au 20, leo ndani ya kitabu hiki cha bajeti Mhe. Waziri anatuahidi ndani ya mwaka 2018/2019 deni hili litakuwa limemaliza kabisa. Kwa kweli hili ni suala kubwa na kwa kweli iko haja ya kuweza kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Rais wa Zanzibar kwa kuweza kusimamia haki ya watu wa Zanzibar na haki imepatikana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ndio nililosema hii ni bajeti ya matumaini. Leo ndani ya bajeti yetu hii serikali kwa kupitia Waziri wa Fedha na Mipango anatuambia tutanunua meli mpya ya mafuta. Meli mpya ya mafuta itanunuliwe ili ile iliyokuwepo iweze kuondolewa, aidha itafutiwe mteja iuzwe au iweze kufanyiwa jambo jengine lolote. Kwa kweli hili ni jambo la matumaini kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Vile vile kuna matumaini na matarajio, inawezekana kwenye bajeti ya mwaka unaokuja tukaweza kununuliwa meli nyengine mpya ya abiria. Ina maana haya ndio yale makusanyo mazuri yanayopatikana moja kwa moja na kwenda kuwanufaisha wananchi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilitaka kulizungumza na haya yote ninayoyazungumza, haya ni mafanikio ya utekelezaji wa ilani ya CCM Zanzibar. Mhe. Spika, moja katika jambo nilofurahi sana katika yale mazingatio maalum, ni kutengeneza makazi bora kwa vikosi vyetu vya SMZ. Mhe. Spika, kwa kweli vikosi vyetu vya SMZ vinafanyakazi kubwa sana hawalali usiku na mchana, sisi tukilala wao ndio wanakuja kutulinda. Lakini ilikuwa ukitembelea kwenye makazi yao yalikuwa hayaridhishi sana, ingawa fedha zilizotengwa hapa ni kidogo na ndio maana nikasema tutajaribu kuishauri serikali maeneo mengine ya kuweza kuongeza fedha ili bajeti ya mwakani vile vile ziweze kuongezwa fedha nyengine zikajenge na zikamalize matatizo ya makazi katika vikosi vyetu vya SMZ. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna jambo ambalo vile vile limetengewa fedha karibu bilioni 8 kwenye bajeti hii, katika suala zima la matayarisho ya Bima ya Afya. Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri wa Afya kwa bahati mbaya hayupo, lakini najua serikali ipo. Suala hili la Bima ya Afya tumeshalizungumza kwa muda mrefu, wananchi wetu wa Zanzibar ni wanyonge hali zao dhoful hali, lakini tukiweza kutengeneza mfumo wa Bima ya Afya basi tutaweza kuwasaidia sana katika kuwapunguzia umaskini. Ile Programu ya Mkuza hapa ndio itakuwa inatekelezwa kwa vitendo. Sasa kwa kuwa suala hili limeshazungumzwa sana, nakuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kaa na Mhe. Waziri wa Afya ili suala hili la Bima ya Afya ndani ya mwaka huu

2017/2018 tuhakikishe wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wote wanatengenezewa utaratibu wa kukatiwa Bima ya Afya ili mfanyakazi aweze kuwa na afya nzuri, aweze kulitumikia taifa na aweze kuzalisha mali zaidi na kuongeza mapato serikalini. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Spika, suala jengine katika mazingatio maalum kusambaza umeme katika visiwa. Mhe. Spika, kwa kweli tunaishukuru sana serikali. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia masuala ya Ardhi, Nishati, kwa kweli tunashukuru visiwa vile ambavyo walikuwa hawajawahi kuuona umeme Fundo kule na Kokota. Sasa hivi tunategemea kisiwa kimoja katika hivyo tayari wameshauona. Haya yote ni mafanikio ya Chama cha Mapinduzi na ni mafanikio ya utekelezaji wa ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine tumeambiwa hapa kwamba kuna fedha karibu 1.5 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha visima vya maji ya umeme. Mhe. Spika, tuliposoma hotuba yetu ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tulieleza katika hotuba yetu ya kamati, kwamba tunaiomba serikali kuhakikisha katika bajeti ya mwaka huu visima vile vinaweza kufanyiwa *installation,* kuunganishwa umeme na miundombinu mingine, ili kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika maeneo yetu ya mijini na vijijini.

Mhe. Spika, naona kama nikiendelea kumwaga sifa kwa serikali, dakika zangu 30 nitazimaliza, itakuwa bado sijaweza kuchangia mchango mwingine wa serikali. Kwa kweli mambo ni mengi sana, lakini tu nilikuwa najaribu kutoa indhari kwa serikali.

Mhe. Spika, huku tumeona katika haya haya mazingatio katika Mfuko wa Miundombinu kuna suala zima la *CCTV Camera*. Mhe. Spika, hapa nataka kueleza kitu ambacho siridhiki nacho sana. Mhe. Spika, leo tunapotaja *CCTV Camera* tunategemea tutakuwa na ulinzi wa kutosha, bado kuna matukio mengi ya uhalifu yanatokezea *CCTV Camera* zimeshaanza kufungwa, lakini bado inakuwa ni tatizo sana kuweza kuwakamata wale wahalifu. Ingawa tunashukuru hivi karibuni yule kijana aliyewachoma choma visu watalii na watu wengine, inategemea hatujui kwamba hizi *CCTV Camera* zilianza kufanyakazi, lakini aliweza kupatikana kwa haraka.

Mhe. Spika, kimsingi bado ukiangalia taa za barabarani tunazowekewa, vile vile ukiangalia na *Traffic Light* Mhe. Spika, naomba sana serikali yetu inapofunga mikataba na haya makampuni waangalie ubora tusiangalie bei, mambo ya kutafuta mambo rahisi matokeo yake kila siku tutapigwa changa la moto.

Mhe. Spika, ukiangalia *Traffic Light* kwa kweli wakati mwengine zinasababisha ajali. Unaweza kwenda sasa hivi taa zinawaka ukirudi baadae taa haziwaki, likipiga wingu la mvua tu hata mvua haijanyesha tayari *Traffic Light* hazifanyi kazi. Sasa maeneo kama haya sisi tukipitisha bajeti tukiingiza fedha matokeo yake tukiona miradi ile haifanyi kazi vizuri kwa kweli tunakuwa haturidhiki kabisa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda moja kwa moja katika kuchangia hiyo Bajeti Kuu ya Serikali. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 8 kifungu cha 17 Mhe. Waziri ameeleza namna gani pato la wananchi la Zanzibar lilivyoongezeka, lakini vile vile akaangalia na matarajio ya idadi ya

watu. Idadi ya watu sasa hivi tunategemewa Zanzibar tutakuwa tunakaribika kufika karibu watu 1,455,000.

Mhe. Spika, ongezeko hili ni kubwa lakini bado naomba tena nianze kutoa indhari kwa serikali, ongezeko hili sisi tunaliona kubwa lakini ongezeko hili litaendelea kuongezeka iwapo pale tu, baada ya Zanzibar kuanza uzalishaji au uchimbaji wa mafuta na gesi. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, katika eneo hili lazima tujitahidi tuwe makini sana katika kupanga mipango ya miji yetu ya Unguja na Pemba. Mheshimiwa tena miji yenyewe mijini na vijijini.

Vile vile hapa ameeleza Mhe. Waziri kwamba pato la mwananchi limekua kutoka mwaka 2015 kwa shilingi 1,633,000 na limeongezeka hadi kufikia shilingi 1,860,000; kwa thamani ya dola alitwambia kwamba, kwa mwaka 2015 ilikuwa pato la mwananchi ni US$ 818, lakini kwa sasa hivi ni US$ 830. Sasa hapa naomba sana watu wachumi na wa takwimu hebu watuweke sawa.

Mhe. Spika, kama ilikuwa dola mwaka 2015 kama ilikuwa thamani ya dola ni shilingi 2000 tukaweza kupata pato la mwananchi sawasawa na dola 818, lakini kwa mwaka huu hivi sasa tunapopitisha hii bajeti tumeambiwa kwamba pato la mwananchi limekua kutoka US$ 818 hadi US$ 830, hii Mhe. Spika, baada ya kukaa na kuangalia nikapiga mahesabu unajua sisi wengine ndio tumesoma kule mbali, baada ya kupiga mahesabu mimi nikagundua kwamba hii thamani ya dola iliyowekwa hapa sio sahihi thamani ya dola kwa sasa hivi ni US$ 809 sio US$ 830. Mimi nimefanya kwa hesabu ya *current price* ambayo iko katika soko sasa hivi. Kwa sababu sasa hivi dola tunainunua karibu kwa shilingi 2,235, sasa ukipiga mahesabu ya haraka haraka utakuta kama dola 809. Sasa hapa ukiangalia ukiifanya kwa thamani ya dola ina maana pato la mwananchi wa Zanzibar litakuwa limeshuka kwa sababu mwaka 2015 ilikuwa US$ 818, mwaka 2017/18 dola imetoka 818 mpaka kuja 809. Sasa hapa aidha labda hizi hesabu ziwe zilifanywa kichumi, lakini kama zilifanywa kama tunavyofanya sisi huko mtaani basi pato la mwananchi limekua.

Kwa sababu hii tunaangalia vipi, tunaangalia na *purchasing power*, unaweza ukawa na shilingi 1,000 mwaka 2000 ukaweza kununua televisheni ya rangi *flat screen inch* 24, lakini unaweza ukawa na shilingi 1,000 wakati huu wa sasa hivi televisheni ile ya inchi 24 ya rangi huipati. Kwa hiyo, tuki-*compare* T.Shs na dola ina maana hapo utagundua kwamba *purchasing power* ya mwananchi wetu imepungua na pato limeshuka. Kwa hivyo, lazima tuhakikishe kwamba serikaliyetu kutokana na ongezeko la idadi ya watu lazima tuhakikishe kwamba tunaongeza mapato ili kuongeza kipato cha mwananchi.

Mhe. Spika, nataka niende haraka haraka. Mheshimiwa tumejaribu kuangalia ukuaji wa uchumi Zanzibar umekua kutoka 6.8 mpaka sasa hivi tunakwenda katika 7.1. Sababu kwa kweli amezieleza Mhe. Waziri sina haja ya kuzieleza, lakini kikubwa ninachotaka kukisema hapa Mhe. Spika, kwamba lazima tuhakikishe tunadhibiti mfumko wa bei, bila ya kudhibiti mfumko wa bei Mheshimiwa kwa kweli mshahara hata tukiongeza kiasi gani utakuwa hauwezi kusaidia. Mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa sababu ahadi zake anazitekeleza, alipoingia madarakani mwaka 2010 alikuta mshahara wa kima cha chini ulikuwa ni shilingi 100,000; lakini ndani ya kipindi chake hichi hajamaliza kipindi chake sasa hivi tayari ameshafika shilingi 300,000 yaani asilimia 300 ameweza kuongeza mshahara. Sasa kitu ambacho ninakiomba Waheshimiwa tujitahidi kuisimamia serikali tuwe wakali ili mapato yaongezeke zaidi ili Mhe. Rais

anapotuletea bajeti yake ya mwaka 2019/2020 tuhakikishe kwamba mshahara wa kima cha chini angalau ufike shilingi 500,000 na kwa *speed* yake hii na kwa mapato jinsi yanavyoongezeka tunategemea tunaweza tukafikia hapo, lakini kuna mambo ambayo ili tuweze kufika hapo lazima tuweze kuyazingatia.

Mhe. Spika, imeelezwa katika suala zima ukurasa wa 9 kifungu cha 22. Hapa pameelezwa namna gani miradi kupitia *ZIPA* ilivyoshuka. Mheshimiwa katika eneo ambalo mimi kila siku huwa ninalizungumza ni eneo hili, leo Mheshimiwa miradi imeshuka kutoka miradi 36 mpaka miradi 16; miradi ambayo ilikuwa na thamani ya US$ karibu 346.8 imeshuka mpaka US$ 150.5. Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha na hii inasababishwa na nini. Mheshimiwa, *ZIPA* kuna urasimu mkubwa, urasimu iliokuweko *ZIPA* kwa kweli sijambo tena la kuweza kulivumilia na kulistahamilila. Mheshimiwa, kuna wawekezaji wanakuja wanataka kuwekeza viwanda, juzi nilisema hapa mwekezaji sasa hivi tokea ameleta maombi yake ya kuwekeza mradi mwezi wa 11 sheria yao *ZIPA* wanasema ndani ya wiki mbili tayari yule mwekezaji awe ameshapatiwa jawabu leo miezi 11 hakuna jawabu yoyote, hakuna mashirikiano baina ya *ZIPA* na taasisi nyengine, hakuna mashirikiano ya *ZIPA* na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wala hakuna mashirikiano ya *ZIPA* na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, hapa tulipitisha sheria tukasema *ZIPA* na iwe *One Stop Centre* na leo Mhe. Waziri alirejea. Mhe. Spika, suala la *One Stop Centre* tumeshalizungumza sana na leo tunalirejea lile lile. *ZIPA* Mhe. Spika, kuna mkubwa mmoja mimi ni rafiki yangu sana, akisafiri yeye wiki mbili *ZIPA* pale hakuna kinachoendelea watu wote wamefunga mikono. Haiwezekani Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Dakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *Allahu Akbar*. Mhe. Spika, mimi naomba sana pamoja na kwamba kuna mapitio ya masuala ya sheria ya *ZIPA* na hivi, naomba hili suala liweze kuzingatiwa kuna miradi mikubwa kama hivi sasa tunasema serikali inatakiwa ili tuweze kukuza uchumi wetu, basi lazima tuitumie vizuri tuwe na *land use plan*.

Mhe. Spika, leo maeneo ya utalii ndio tunaishi sisi, maeneo ya kilimo ndio tunaishi sisi, uchumi kwa kweli hauwezi kukua hata kidogo. Sasa kitu ninachokishauri Mhe. Spika, sasa hivi ni lazima tu-*review* sera zetu za ardhi tuangalie yale maeneo hata kama kuna makaazi ya watu, yale maeneo ambayo ni *potential* kwa uwekezaji hasa utalii, basi serikali kwa kupitia shirika la nyumba na taasisi nyengine ziwajengee wananchi wale nyumba za kisasa bora kuwaondoa kule katika maeneo ya utalii, ili yale maeneo yabakie ni maeneo ya utalii ili kuongeza mapato ya serikali.

Lakini jengine Mhe. Spika, katika hili hili kuhusu misamaha ya kodi kamati ilizungumza. Leo serikali ndani ya sheria, kuna sheria inayowavutia wawekezaji kuwapa misamaha ya kodi. Wawekezaji wale wakishafika Mhe. Spika, kodi zinakuwa nyingi hawajui wafanye nini.

Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri ndugu zetu wawekezaji wa *Penny Royal*. Mhe. Spika, wengi wanasema Hamza Hassan *Penny Royal* ana hisa. Mimi sina hisa hata moja, mimi nimevutiwa na mradi wao, kitu ambacho ninakiomba serikali i-*play the role*, serikali chukuweni nafasi yenu, yale maeneo ambayo mliwaahidi mtawapa wayapate wale msiwapeleke kwa

wananchi, serikali imalizane na wananchi ili wale wenzetu wawekezaji watumie maeneo yale ya wawekezaji kuweza kuwekeza mradi ambao utaongeza mapato kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kweli kama nilivyozungumza muda wetu kwa kweli umejibana sana lakini tuna mambo mengi ya kuishauri serikali, tutapitia katika njia nyengine ili kuweza kuhakikisha Mhe. Waziri tunamsaidia. Lakini pia naomba takwimu Mhe. Spika. Samahani hili la mwisho. Takwimu Mhe. Spika, naomba wenzetu Wizara ya Fedha na Mipango wanapotuletea takwimu basi wawe makini sana. Nimeangalia kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango katika ukurasa wa 23, hiki kitabu cha hali ya uchumi. Ukurasa wa 23 nimejaribu kufanya *comparison* na kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Wanawake na Watoto hakilingani kabisa takwimu zake, nitaomba nimalize hizi takwimu halafu nikae kitako ili waende wakafanye masahihisho.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 46 kinasema "Jumla ya malalamiko 143 Unguja 87 na Pemba 56 yamepokelewa na kupatiwa ushauri maelekezi kama hivi ifuatavyo".

1) Madai ya mahari ni 5 kwenye kitabu cha wanawake na watoto kinasema 7.
2) kesi za kupigwa 22 kitabu cha Wanawake na watoto kinasema 28.
3) Kutoroshwa 3 Kitabu wa Wanawake na watoto kinasema 7.
4) Migogoro ya ndoa 22 kitabu cha wanawake na watoto kinasema 19.
5) Madai ya mali baada ya kuachana humu wanasema 11 lakini kwenye kitabu cha wanawake na watoto ni 2.
6) Kutelekezwa na wanaume 50 kwenye kitabu cha Wizara ya Fedha lakini wanawake na watoto ni 58.
7) Madai ya Mashamba ni 5.
8) Halafu hii ya kushangaza sana kesi ya kubakwa ni moja Mhe. Spika, mawio kila siku ukisikiliza vitoto vidogo vya miaka miwili vimebakwa, leo ndani ya Kitabu cha bajeti ya Wizara ya Fedha kinasema kesi ya kubaka ni moja haya yapo mengi.
9) Migogoro ya ardhi wanasema 2 kwenye kitabu cha Wanawake na watoto ni 5.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa Hamza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sasa Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuchambua takwimu wanapotuletea hivi vitabu Mhe. Spika, sisi tunapoteza muda wetu tunakaa tunavisoma, kwa hvyo naomba sana takwimu hizi ziweze kurekebishwa na kwa sababu gani hotuba za Wizara zote zimeshapita hii ina maana ndio hotuba mama hii haina vifungu hii, hii unauliza tu mmeikubali ndio mmeikataa ndio. Sasa kama itakuwa takwimu zinatofautiana…..

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja Ahsante sana. (Makofi)

Mhe. Spika: Ahsante sana sasa naomba nimuite Mhe. Khadija Omar Kibano atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Maryam Thani Juma ajiandae.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijaalia nikapata kidogo na mimi kuchangia mawili matatu niliyonayo katika bajeti hii ya fedha. Kwanza namshukuru Rais wangu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa umahiri wake na kazi zake anazozifanya katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nataka niende moja kwa moja katika ongezeko la elimu, ongezeko la elimu katika skuli yangu ya Kokota kuna madarasa sasa hivi yameshaongezeka kwa sababu kule kulikuwa kuna madarasa matatu mpaka darasa la nne, lakini sasa hivi katika mwaka huu wameongezeka madarasa mawili na kutoka na hali ya madarasa ni kidogo sana kwa elimu ilivyoongezeka, kwa sababu kule kulikuwa kwanza ni ukosefu wa elimu ulikuwa hakuna lakini watu wameshajihika vizuri na wanaendelea na kusoma vizuri alhamdullillahi kwa Mwenyezi Mungu anawajaalia katika elimu wameshaendelea vizuri sana. Kwa hivyo naiomba Wizara au Serikali katika mapato haya na bajeti hii ili ile skuli iongezeke katika masuala ya elimu, kwa hivyo naiomba Serikali ifanye shughuli zake kama inavyopangwa katika bajeti hii ya mara hii.

Nikitoka hapo naingia katika Wizara ya Afya, Wizara ya afya katika vituo vya uzazi vituo vyetu vya uzazi katika Jimbo langu la Mtambwe nashukuru sana Wizara na Serikali imenipatia katika jimbo la Mtambwe kuna vituo viwili vya uzazi kimoja Mzambarauni, na kimoja kipo Mtambwe Uondwe vituo hivi nashukuru vipo katika eneo langu na sasa hivi tayari kimoja kimeshaanza kufanya kazi, lakini vina ukosefu wa wahudumu au wakunga pale ni kidogo sana kutokana na hali iliyopo. Kwanza hichi kituo cha Uondwe kimefunguliwa hivi karibuni lakini mpaka sasa hivi vifaa vyake kabisa vimeshakamilika bado wahudumu wa wazazi pale hawapo halafu waajiriwa ni kidogo sana kwa sababu pana mhudumu mmoja tu pale mwanamama anayeshughulikia na masuala haya waliobakisha wote ni *ma-orderly*.

Kwa hivyo naomba vile vituo vifanye kazi yake kama vilivyopangwa Wizara hii au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wapeleke wafanyakazi hawa katika vituo vile ili tuondokane na ule uchangamoto zilizokuwepo katika masuala yetu ya uzazi.

Sasa nakwenda katika suala langu la nishati kwenye Wizara ya Nishati na maji nashukuru mpaka sasa hivi katika Wizara ya Fedha na Wizara zote ili kunisaidia katika kupeleka umeme katika kisiwa changu cha Kokota hilo nalishukuru na nampongeza Waziri wa Nishati na Maji katika kunisaidia, na hivi sasa nipo katika mchakato wa kutupelekea maji katika kijiji kile.

Lakini nina changamoto yangu vile vile nina kijiji changu cha Kinazini/Mtambwe, Makoongeni bado wananchi wangu wanadhalilika kwa maji na umeme tangu enzi za Karume hadi hii leo wanatumia visima vya maji ya kawaida, mwaka 2015/2016 waliingiliwa na maradhi ya *Typhoid* kutokana na usumbufu wa maji wanayokuwa wanayatumia. Kwa hivyo naomba Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi, Nishati na Maji vijiji hivi bado vina usumbufu wa matumizi yale yale ya zamani wanakuwa hawajapata huduma za kisasa, naomba miundombinu hii ifanyiwe kazi kama inavyopangwa katika bajeti hii, kama haikuwa mwaka huu lakini japo mwakani tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu munisaidie katika vijiji vyangu hivi.

Nikitoka katika Wizara hiyo nakuja zangu moja kwa moja katika Wizara ya Biashara, Wizara ya Biashara niko katika zao la karafuu sasa hivi ni kubwa zana katika nchi yetu tunalolitegemea kama Pemba na Unguja, hili zao la karafuu linalozalishwa katika Visiwa vyetu vya Pemba zaidi

kuliko Unguja kwa hivyo nahitaji Wizara hii ya Biashara katika kwenda kukodisha mashamba yao ya karafuu kama ni Wizara ya Kilimo, ikiwa ni wahusika wenyewe wanaohusika katika masuala haya wale watakaokwenda kukodishwa mashamba hawa wawe ni watu waadilifu, wasikodishwe watu waliokuwa sio waadilifu kwa sababu zao letu linapotea sana ndio ukaona mara nyingi karafuu zinakwenda kwenye magendo kutokana na wanaokodishwa sio waadilifu kwa hivyo wasilifumbie macho suala hili, walisimamie kwa uangalifu ili wananchi na Serikali yetu ipate mapato ya ndani. Kwa sababu mpaka sasa hivi kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado tunatumia kipato chetu cha nchi yetu hatutegemei wahisani walioko nje tupo hapa hapa nchini kwetu Zanzibar tunatumia mazao yetu.

Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Wanawake na Watoto hapa ninachangia katika masuala ya jinsia, suala la jinsia mpaka sasa bado ni changamoto kubwa sana hasa watoto wadogo hawa wanakuwa wanadhalilika vibaya sana, ukiendelea katika masuala yetu mayatima, watoto waliokuwa na mzazi mmoja japokuwa hakuna mtu anaezaa peke yake ni mashirikiano lakini yule aliyekuwa anatupiwa ule uzazi kuna hawa kinamama wanaotekelezwa. Lakini hizi kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma mimi nasema Wizara haifuatilii vizuri takwimu zake na mashirikiano pamoja na watendaji wao, ikiwa watashirikiana na watendaji wao hizi kesi ni nyingi sana sana mimi nilikuwa ni mratibu wa wanawake na watoto pale Wilaya ya Wete tu tulikuwa tukikamata kesi chungu nzima na tukiangalia katika takwimu ya majumuisho kunakuwa na kesi kidogo sana.

Kuna miaka ya nyuma tulikuwa tukikamata kesi kama hizi na hivi sasa imezidi zaidi maradugu, halafu nikienda ubakaji wa walimu wa Wizara ya Elimu, jamani tusiseme kwamba Wizara ya Elimu walimu hawabaki wanawabaka watoto vibaya sana, hilo mimi nalizungumza hapa katika Baraza letu tukufu. Kama ni takwimu ya mwaka huu 2016 basi na 2017 hii miaka ya nyuma kesi zipo Mahakamani japo hapa hazitakiwi zielezwe lakini zipo Mahakamani na wapo walimu wanaofanya haya matendo, walimu wa vyuoni, walimu wa madrasa haya masuala wanayatekeleza. Kwa hivyo mimi nazungumza Wizara zitafute takwimu zake katika kesi zinazoendelea katika madawati ya afya, madawati ya wanawake, madawati ya vituo vya Polisi wazisimamie.

Nikiendelea nakuja kwenye vikosi vyetu vya SMZ kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma vikosi vya SMZ makazi yao ni mabaya, mimi katika Wilaya yangu ya Wete zamani nilikuwa nikisema majumba yale yote ni majumba ya magereza, lakini kumbe zile nyumba zina mchanganyiko wa vikosi tofauti tofauti wanaishi pale, kwa hivyo nyumba za magereza ni kidogo sana zinazoishi watu pale hata zile ofisi zao hazitoshelezi. Kwa hivyo naomba Wizara ya Fedha watu hawa waendelezwe wajengewe majumba yao wawekwe katika makazi mazuri, kwa sababu yale makazi sio mazuri sana wanayokuwa wanaishi katika vikosi vyetu hivi tunawadhalilisha upande mmoja, kwa hivyo ninachokiomba Wizara ya Fedha ikiwa imeshatoa mapato yao tayari watu wafanyiwe kazi kama wanavyopaswa kiserikali inavyozungumza sio ya kuwa wao wakae kitako kwenda kufanya shughuli nyingine.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono hotuba hii kwa mazungumzo yangu niliyozungumza madogo kwa hivyo naunga mkono asilimia katika hotuba hii angalau na mimi nimechangia kidogo kidogo katika masuala haya. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa sasa naomba nimuite Mhe. Machano Othman Said, atafuatiwa na Mhe. Maryam Thani Juma na Mhe. Simai Mohammed Said ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na rehema zake kufanya leo hii kufika hapa kuchangia bajeti hii kuu ya serikali. Pili nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha bajeti hii nzuri ya serikali najua ni kazi kubwa sana amefanya yeye na watendaji wake, na leo hii sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaichangia na kuisaidia serikali yetu. Pia nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na niwashukuru na kuwapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa kuendeleza vyema swaumu katika mwezi huu mtukufu kwa amani na kwa mashirikiano kwa dini zote zilizokuwepo Zanzibar wanaiheshimu sana Ramadhani, na naomba waendelee kushikamana ili nchi yetu iweze kuendelea.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais kwa uteuzi wake kwa Makamanda wawili wa JKU, Kamanda Ali Mtumweni na pia Kamishna Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ndugu Ali Abdalla Ali. Matarajio yangu kwamba Wakuu hawa wa Vikosi watafanya kazi vizuri kwa niaba ya serikali kuwahudumia wananchi lakini pia kuimarisha maslahi na uwezo wa vikosi vyetu. Baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wamezungumzia umuhimu wa kuimarisha vikosi hivi kuanzia makaazi, vifaa vya kutendea kazi na mafunzo ili waweze kukabiliana na changamoto ambazo zipo.

Mhe. Spika, nianze kuchangia bajeti hii kwanza kwa kuipongeza serikali katika mwaka huu ambao tunamalizia wa bajeti mwaka 2016/2017. Mheshimiwa kinyume na miaka ya nyuma serikali imejitahidi sana kupeleka fedha za matumizi katika mawizara. Mimi hapa nasimamia wizara mbili katika pitapita yangu katika wizara na kamati yangu nimeona kwamba karibu asilimia 80 mpaka 99 sasa hivi wengine wamepata fedha za matumizi kwenye wizara. Hili sio jambo dogo ni kazi kubwa ya serikali lakini na Mhe. Rais pia na ufanisi na utendaji wa Waziri wa Fedha. Kwa hivyo, tunasema Mhe. Waziri hongera sana.

Mhe. Spika, kwa bajeti hii ambayo tunatarajiwa kuianza kesho kutwa Julai matarajio yetu kwamba wizara zitaongezwa matumizi lakini pia na kuingiziwa fedha. Juzi nilimsikia mchambuzi mmoja wa bajeti lakini ni mpinzani nilisoma kwenye gazeti, akasema bajeti hii matumizi ya kawaida ni makubwa sana kuliko ya maendeleo. Lakini sijawahi kusikia nchi ya Afrika ambayo ina matumizi makubwa ya maendeleo kuliko matumizi ya kawaida. Kwa hivyo, hili ni jambo la kawaida kwa serikali, matumizi ya kawaida yanakuwa ni makubwa kwa huku kwetu. Kwa hivyo, hilo wala lisiwavunje moyo serikali huu ni utaratibu wa kawaida na naomba mimi waendelee na utaratibu ilimradi wajidhatiti katika ukusanyaji wa mapato lakini pia wafanye *location* nzuri za mgawanyo wa fedha katika taasisi za serikali na wasimamie matumizi ya serikali ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wananufaika na wanasonga mbele katika juhudi za kuleta maendeleo.

Mhe. Spika, lipo tatizo bado dogo linaendelea kubwa na dogo, lakini linaendelea ila bahati nzuri serikali kupitia Wizara ya Fedha wanajitahidi sana, la kuhakikisha kwamba kila mwananchi wa Zanzibar anayestahiki alipe kodi ambayo amepangiwa kulipa. Mheshimiwa pamoja na kodi lakini kukusanya mapato katika vyanzo mbali mbali, na nimefurahi kwamba serikali

imezungumza kuwa wanatarajia kuwa na utaratibu mpya wa malipo kwani *e-government* itaanza kutumika zaidi katika ZRB. Si vyema mwenye hoteli leo kwamba achukue *cash* aende ZRB akachukue *slip* aende benki akalipe, wawe na utaratibu hata kama yuko kwenye hoteli aonekane analipa fedha na fedha sahihi zinapatikana kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Nafikiri tukijipanga vizuri tunaweza kuwa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, nizungumzie sekta ya utalii, sekta hii ni sekta muhimu sana katika ukuzaji wa uchumi wa Zanzibar na ina mapato makubwa. Mapato makubwa yenyewe kwanza kodi na matumizi ya watalii lakini pia sehemu ya ajira kwa wananchi wetu wa Zanzibar ambao wameajiriwa katika sekta ya watalii ni wananchi wengi na hao wanasababisha kipato kwa wananchi wenzao wa Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, pamoja na kwamba tuna umuhimu wa watalii kuna mambo mimi bado yananisikitisha.

Jambo la kwanza na naiomba serikali ilione kwamba hili ni jambo la msingi, maradhi ya kipindupindu Mheshimiwa yanaturudisha nyuma sana. Na ni kama aibu kwetu sisi Zanzibar kwamba kila mwaka na kila ikinyesha mvua tunapata kipindupindu, hebu tukae chini tuangalie tutafanyaje ili kuondoa kipindupindu Zanzibar isiwe tatizo. Tunayajua maeneo fulani kuna maeneo hasa ikinyesha mvua unajua kwamba sehemu fulani itatoa kipindupindu, yaani kama uzalishaji sasa hivi kila mvua sehemu fulani ina kipindupindu, kila mvua sehemu fulani ina kipindupindu. Mheshimiwa na kipindupindu asilimia kubwa au asili yake kubwa ni uchafu.

Mhe. Spika, sasa serikali waone kwamba hili ni tatizo isiwe tunasemwa sana duniani, yaani tunasemwa kwamba Zanzibar kila ikinyesha mvua kipindupindu nchi yenyewe ni ndogo hawawezi kumaliza kipindupindu kwa nini tufikie hapo. Mheshimiwa pia kuna maeneo watu wamelundikana sana wamehamia sana ndio ambayo yanaleta kipindupindu, hebu tukae vizuri tuangalie mtu anawezaje kuishi hana choo, anawezaje kujenga nyumba ashindwe kujenga choo, kwamba choo hakukitilia umuhimu na lazima tuhakikishe kwamba kila mtu mimi naomba Waziri Wizara ya Ardhi na Wizara ya Nyumba wahakikishe kila mtu akijenga nyumba lazima awe na choo, isiwe unajenga nyumba choo huna unataka upitishe kwenye mto haiwezekani.

Kwa hivyo Mhe. Spika, na hili linasababisha watalii kuwa hawaji vizuri lakini pia linasababisha wananchi wetu wengine wanaotafuta riziki waikose, kwa sababu kama sasa hivi mama ntilie kazuiliwa, wenye mahoteli wadogo wadogo wamezuiliwa, sisi tunaofutarisha waheshimiwa haturuhusiwi. Kwa hiviyo mambo mengi yanakuja kutokana na kipindupindu kukiachia kuwepo Zanzibar kwa hivyo nafikiria Serikali ichukue hatua zake.

Lakini la pili sehemu kubwa ya watalii nao wanakuja Mji Mkongwe ukiangalia Mhe. Spika, hadi leo Beit-el-Ajaib haliko katika hali nzuri, lakini ukiangalia *People Palace* pale kuna sehemu mbili, kuna sehemu moja ya Waheshimiwa kina Shehe Juma hapa *BLM* na sehemu nyengine ndio Makumbusho pale, ukiangalia tu nje unaona *BLM* iko vizuri inang'ara lakini upande wa pili hautazamiki ambao ndio wanaingia watalii. Sasa Serikali labda ichukue juhudi na ule upande wa pili wa *People Palace* waufanyie ukarabati ili upendeze na uvutie watalii na pale wanakwenda watalii wengi, kwa hivyo Mhe. Spika, hili nalo Serikali waone kwamba ni moja ya chanzo cha utalii.

Lakini la tatu amani katika nchi yetu juzi tumesikia kujeruhiwa wale wageni kama si picha na Wazanzibari wengine ilikuwa ni *issue* kubwa sana, bahati nzuri tunaishukuru Serikali kwamba kwa juhudi zake yule aliyefanya uhalifu ule amekamatwa lakini ingelikuwa hatua mbaya sana.

La nne idadi, idadi ya watalii Mheshimiwa inakuwa inaleta kizungumkuti kwenye kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha inazungumzia kwamba kuna watalii karibu 376,424 lakini tuaona bado idadi ndogo watalii ambao wanaingia Tanzania karibu robo na nusu na Zanzibar wanakuja na wenzetu upande wa Bara watalii zaidi ya 1,500,000 wanaingia sisi hata laki tano tunashindwa kuwa wamefika mpaka leo. Mheshimiwa idadi ya watalii bado ina mashaka mimi niliwahi kutembelea na kamati yangu Kaskazini, tulipofanya kikao cha maafisa wa Kaskazini na Mkuu wa Mkoa bahati nzuri alikuwepo na Afisa Utalii wa Mkoa, tukamuuliza kwa mwaka unapokea watalii wangapi katika Mkoa huu wa Kaskazini haijui idadi ya watu ambao wanakwenda Kaskazini kama watalii (wageni), sasa huyo Afisa wa Utalii wa Mkoa hawajui watalii wanaoingia katika Mkoa wake pengine na Kusini hivyo hivyo, pengine na Pemba hivyo hivyo tutawajuwaje watii hawa jamani Mhe. Waziri fanyeni mipango tuhakikishe kwamba idadi ya watalii inakuwa na tunajua matumizi na mapato yote ya utalii. *(Makofi)*

Nikitoka hapo nije Sekta ya Miundo mbinu kwanza barabara, Mhe. Spika, bahati nzuri uliwahi kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa hivyo barabara unazidua vizuri na mimi nimepitia huko pia, mvua hizi za masika zimeharibu sana barabara zetu zikiwemo za mijini na vijijini, mimi naomba Mheshimiwa tuweke nguvu sana zile barabara zirejeshwe katika hali yake ya kawaida na sikuangalia sijaona mabadiliko ya *road fund* lakini *road fund.* Mheshimiwa imefika wakati wake nayo iangaliwe upya, tusipoimarisha *road fund* mzigo wa matengenezo ya barabara unaweza kuwa mkubwa sana, na jambo jengine Mhe. Spika, namuomba Mhe. Fedha kwa sababu yeye ndio mwenye *road fund* pamoja na kuzitumia fedha za *road fund* kwa ujenzi na matengenezo, hebu waangalie na ununuzi wa vifaa vipya vya kutengeneza barabara katika Idara ya UUB.

Mheshimiwa wale UUB wana tatizo kubwa la vifaa, nafikiri wana *pair* moja tu ya kazi humu waheshimiwa hata kukiwa na kazi ndogo dogo za kufanya utakuwa na fedha mfukoni lakini vitendea kazi na UUB ni kishindo hawawezi kwa sababu hawana fedha, hawana vifaa. Sasa Mhe. Spika, Serikali ione hata kwa kukopa kufanya tuliposamehewa madeni ndio tulipata vifaa vya mwisho vya kufikia UUB msamaha wa madeni wa Tanzania ule tukapata gari na vifaa vyengine, kwa hivyo sasa na Serikali ione kwa kupitia *road fund* kwamba vifaa UUB vinatafutwa ili ujenzi wa barabara hasa *feeder road* ziweze kutengenezwa.

Mhe. Spika, umeme nalo hili sekta muhimu sana nilipochangia Wizara ya Ardhi, Nishati na Mazingira niliiomba Serikali iangalie uwezekano wa kulipunguzia kazi Shirika la Umeme, tuanzishe Kitengo kama cha wenzetu Bara cha REA cha kusambaza umeme vijijini na mijini, baada ya kuwaachia Shirika la Umeme. Shirika la Umeme waendelee kuwa na kazi ya kuuza umeme na mambo mengine ya kitaalamu lakini mambo kama uwekaji nguzo nyaya za umeme hii itafutiwe kitu kingine. Mheshimiwa hili tunaliweza, kwa sababu sasa hivi tuna *two percent* ya kodi ya miundo mbinu ya Shirika la Umeme kila tukinunua umeme, tuanzishwe kitengo halafu zile fedha wapewe wao waanze kushughulikia.

Jengine Mheshimiwa maji nalo hili narejea tena umefika wakati kwa Serikali kuangalia uwezekano na maji nayo kupeleka katika ukatuzi, niliuliza swali juzi kwa Waziri wa Maji kwamba ni kiasi gani cha fedha kimetumika kuanzia mwaka 2000 mpaka 2017. Jibu ambalo limekuja ni bilioni 178,251,400, bilioni 178 za maji zimetumika Zanzibar ni fedha nyingi sana Serikali wametowa lakini kila mwakilishi na kila mwananchi kila jimbo wanalalamika tatizo la maji safi na salama tujiulize fedha hizi zote zimetumika wapi je, tumefeli katika miradi hii ya maji fedha nyingi Mheshimiwa sasa mimi kwa kuionea huruma Serikali mimi nafikiria wakati umefika nao, hebu tuijaribu hii taasisi ya maji kuipeleka katika Halmashauri za Wilaya ili kila Halmashauri ionekane *capacity* yake ikoje maji na mimi nina hakika kwa fedha hizi tunazozipata kwa maji ikipelekwa huko baada ya miaka miwili, mitatu hakuna Wilaya au jimbo litalalamika suala la maji. *(Makofi)*

Lakini kama tutaendelea kuwa na ZAWA kama ilivyo sasa tutazitumia fedha hizi mara mbili na tutakuwa hatuna maendeleo yoyote ya maji, lakini mimi naona hata sisi wananchi tunalalamika ulipaji wa ada za maji lakini hata ikianzishwa tozo la maji kwenye bei ya mafuta au nini, inaweza kutusaidia na tukaweza kwenda mbele na tukamaliza tatizo la maji.

Mheshimiwa nije katika elimu hapa niombe kwamba wa uangalie sana Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa huu una wanafunzi wengi sana skuli zina wanafunzi wengi baadhi ya skuli zina wanafunzi mpaka 130 kwa darasa naipongeza juhudi ya Serikali kujenga skuli maalum katika maeneo kwa wilaya, lakini bado tatizo ni kubwa sana.

La mwisho, mwisho Mheshimiwa nizungumzie mambo mawili kwanza umeme, bei ya umeme nilitaka tu Mhe. Waziri pengine Mhe. Waziri wa Fedha na atasaidiwa na Waziri wa Ardhi watupe ufafanuzi yapo madai kwamba umeme ambao tunauziwa kutoka *TANESCO* tunauziwa pamoja na ada ya *REA* na ada ya *EURA*, tulitaka kujua ni kweli wanatuwekea ada ya *REA* na EURA maana miradi yote miwili *REA* sisi Zanzibar hatumo na *EURA* haihusiani na Zanzibar, kama ni kweli ina maana hapa tunaweza tukapata fedha baada ya kuzungumza na wenzetu Bara tukazitumia kwa tozo kwa bei hizi za umeme kwenye maji na miundo mbinu mipya ya umeme kama ni kweli kama si kweli itakuwa hakuna jambo jengine.

Lakini la mwisho kabisa ni la kuipongeza Serikali katika utoaji wa misamaha katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani wa mchele, unga na sukari nilitarajia na tende ingelikuwemo katika msamaha wa kodi, sijui kama imo nayo tende *zero percent*, lakini lipo tatizo sisi watumiaji hatujaona tofauti ya bei ya miezi mengine ya kula mchana na bei ambayo tunauziwa Ramadhani. Sasa tunajiuliza hii kodi ina malengo gani? Lengo la kodi hii kuwanufaisha wafanya biashara waigiziaji tu, au walaji wananchi na pengine Serikali wangelitwambia kwa kupitia Wizara ya Biashara na Wizara ya Fedha ni bidhaa gani ambayo katika Mwezi wa Ramadhani imeshuka bei.

Maana mtu anaweza kuwa unamsamehe kodi ya bilioni tatu lakini kaja kutoa msaada kwenye TV ya kakupa vipolo 200 ikaonekana yule mtu mwema sana lakini wananchi kule wameumia na yeye kakusanya fedha nyingi. Kwa hivyo ni jambo jema na tunaomba utamaduni huu uendelee Zanzibar, lakini lazma Serikali iwa-*monitor* hawa wafanyabiashara wanaosamehewa kodi ijuwe kwanza tani gani na najua hilo wanalijua na hizi zimeuzwa kwa muda gani na bei imeshuka kwa kiasi gani. Bila ya kushuka bei ina maana wananchi wa Zanzibar watakuwa bora wangeliona ile

kodi ichukuliwe ipelekwe kwenye Afya na Elimu na ipelekwe kwenye maji, lakini kama watakuwa wanapunguza bei hili ni jambo jema na linastahiki.

Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitamke wazi kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100 namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa juhudi zake, tangu kama Waziri wa Fedha pale mabadiliko yanaonekana wazi wazi, na nafikiri hakuna hata mmoja humu ndani mwenye mashaka na uwezo wa Waziri wetu wa Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nashukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Machano Othaman kwa mchango wako sasa naomba kumwita Mhe. Maryam Thani Juma atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Bahati Khamis Kombo kama muda utaruhusu ajiandae.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika Bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* aliyenijaalia kuweza kusimama, hapa tukiwa leo tuko katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani siku ya 21 nawaomba waislamu wote walimalize kumi hili kwa salama na amani kama *allah* alivyotuhimiza.

Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye ukurasa 39 aya 81 naomba niisome Mhe. Spika aya hii imesema “ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa madarasa jitihada maalum pia zinawekwa katika kumaliza madarasa yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi”.

Mhe. Spika, naipongeza sana Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada hii iliyofikia na kuona kwamba wananchi nao wanajitahidi kwa hali na mali, kuiunga mkono Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye suala hili kwamba mimi naishauri, Serikali kwa mpango huu wa sasa naomba ielekeze nguvu kwa ujenzi wa skuli za ghorofa. Mhe. Spika, hili ni muhimu sana kwa sababu tumeona kwamba Zanzibar maeneo yetu ni kidogo kulikoni wenzetu wa Tanzania Bara, kwa hivyo naomba kwamba ielekeze nguvu kwa ujenzi wa skuli za ghorofa kwa kila eneo ili kuendeleza azma njema ya matumizi mazuri ya ardhi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tukiendelea kutokuweka mfumo katika majengo haya ya Serikali itafikia pahala tuje tukose maeneo ya ujenzi ya madarasa kama hatujafanya ujenzi huu wa maskuli yetu ya ghorofa. Kwa hivyo nimwambie Mhe. Waziri kama tutakubaliana na mpango huu wa ujenzi wa skuli za ghorofa basi Serikali itowe huo mpango wa nchi nzima, ili wananchi wanapotaka kuunga mkono jitihada ya Serikali yao, mpango huu utumike ili tuepukane na upotevu wa ardhi zetu.

Mhe. Spika, vile vile, nielekee katika ukurasa 42 ambao umesema kwamba kipengele hichi mapendekezo ya hatua za kuimarisha mapato. Kwanza kabisa napenda kuipongeza sana Wizara hii kwa hatua ya kuimarisha mapato ya nchi, napenda niipongeze sana Wizara hii ya Fedha

pamoja na watendaji wake lakini Mhe. Waziri hatua hii ni ngumu sana kwa sababu Serikali haijaweka mfumo madhubuti katika kukusanya kodi zake kwenye maeneo mengi.

Mhe. Spika, yapo maeneo mengi katika uwekezaji, tunakosa ada zetu kwa vile bado hatujajipanga vyema kwa maeneo ya uhaulishaji, Mhe. Spika, maeneo haya ya uhaulishaji yamauziano ya mahoteli kutoka kwa mmiliki wa mwanzo kwenda kwa mmiliki wa pili ambaye ni mmiliki mpya, lakini pia ikitokezea kubadilishana utawala wa uendeshaji wa uwekezaji Mhe. Waziri nakuomba katika eneo hili pamoja na watendaji wako wate wa Wizara hii, tuekee mkakati madhubuti ya mapato ya eneo hili yaje kuongeza uchumi katika nchi yetu. Kwa sababu masuala haya ya mapato ni muhimu sana na ndio yanayoongezea mapato nchi yetu. Mhe. Waziri utakapokuja fanya majumuisho naomba uniambie Serikali imejipanga vipi katika kuokoa fedha hizi, lakini pia niambie ni changamoto zipi zinazotukwamisha kuyapata mapato haya.

Mhe. Spika vile vile, Mhe. Waziri katika kuimarisha mapato yetu ni lazima kwanza udhibiti wa vianzio vya mapato tulivyonavyo kabla ya kuanzisha vipya. Mhe. Spika, tumeona bado tunakosa uhalisia katika kukusanya kodi katika vianzio vyetu tunalivyonavyo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri kutokana na haya kwa kulenga walipa kodi tulionao wanalazimika kupeleka mrejesho wa mauziano ili kulipa kodi inayotokana na wananchi wetu, bila ya uhalisia wa mauziano yao au mauzo hayo naiomba Serikali kukamilisha mfumo madhubuti ili kuweza kukusanya mapato ya kukuza uchumi na pato la taifa letu.

Mhe. Spika, mwisho katika eneo hili niseme kwamba Mhe. Waziri uniambie mikakati madhubuti iliyopangwa na Serikali kabla ya Matumizi ya ASB.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa huu wa 28 kipa umbele ya Kitaifa, Mhe. Spika, katika kipaumbele vya kitaifa naomba nizungumzie suala la kuimarisha huduma za kijamii katika huduma ya afya, naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake zilizoonesha kwamba afya sasa hivi zimekuwa ni kipa umbele tukiona Zanzibar tumeimarika kiafya ikawa hatujafikia malengo lakini tuko mbali, tunamshukuru sana Waziri kwa jitihada yake. Katika hatua hii naipongeza Serikali kwamba kwa kuendelea kuwajali wananchi wake kwa kutoa huduma za afya ipasavyo ila lipo tatizo ambalo linatugharimu sana kwa matibabu makubwa ambayo, inatulazimu kuwasafirisha wagonjwa wetu Mhe. Spika, kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Waziri nilipokuwa naipitia Ilani ya CCM niliona azma ya Serikali ya ujenzi wa hospitali kubwa ya Tunguu, Mhe. Spika, hiyo ndio jitihada kubwa ambayo tumeona imeonesha katika ilani yetu ambayo inaondosha azma ya Serikali kwa kiasi kikubwa ya kuwasafirisha wagonjwa nje ya nchi. Mhe. Waziri nataka kujua ni lini itaanza ujenzi huu wa hospitali ili kuokoa zile fedha ambazo zinatumika katika kuokoga wananchi wetu pale tu napowasafirisha kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

Mhe. Spika, napenda niipongeze tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake kuhakikisha kwamba Kisiwa cha Fundo mpaka sasa umefika umeme ingawa haujaanza matumizi lakini hatua nzuri ya Serikali iliyofanywa katika Kisiwa kile cha Fundo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni jitihada nzuri ya Mhe. Rais ambayo ameonesha bila ya kujali itikadi ya kisiasa, bila ya kujali wananchi wa Fundo ni nani lakini Mhe. Rais amejitahidi kwa jitihada yake kuonesha kwamba na Kisiwa cha Fundo wamefikishiwa umeme. Mhe. Spika, niwaombe tu wananchi wa Fundo waupokee umeme ule kwa ajili Mhe. Rais ana imani na wananchi wote wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niende kwenye suala la maji, Suala la maji ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu ya Zanzibar na tunayo maeneo mengi ambayo maji bado mpaka sasa hajafika na bado watu wanatumia visima vile vile vya zamani. Lakini pia Mhe. Spika, suala la maji wanaopata tabu sana kutafuta maji ni wanawake na wanawake hawa na wao wanataka wafaidi matunda ya Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar, vile vijiji ambavyo havijafikishiwa maji.

Mhe. Spika, naomba ninukuu maneno ya mshairi ambayo amesema "maji yakiadimika viumbe tuko tabuni" tena Mhe. Spika, mshairi aliendelea kusema "chai haijapigika kwa sukari na majani sharti maji kuchemka yaone sufuriani ndio utapotosheka ukaitia bulini, maji yakiadimika viumbe tuko tabuni". *(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba sana Serikali ijitahidi kuwapelekea wananchi wetu maji kwa sababu maji ni uhai kwa wananchi wote, baada ya hayo machache naunga mkono bajeti hii asilimia 100 ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Maryam Thani Juma sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said atafuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa hotuba nzuri waliotoa kwa niaba.

Lakini pia Mhe. Spika, nitangulize maeneo yangu ya kumpa pole Mwakilishi jembe wa wananchi wa jimbo la Chake Chake kwa kufiwa na Katibu wetu wa jimbo wa Chama cha Mapinduzi *Inalillahi Waina ilayhi Raji'uun.*

Mhe. Spika, baada ya hapo niende kwenye mchango wangu moja kwa moja, kwanza niseme maneno mazito. La kwanza mara nyingi humu ndani sisi hutupongeza serikali katika mambo makubwa hasa katika kipindi cha Bajeti. Lakini kwa mwaka huu Baraza lako tukufu linastahiki sifa za pekee. Pongeze hizi ziende kwako wewe mwenyewe kwa kuwa kiongozi wetu, kwa mara ya kwanza Baraza la Wawakilishi tangu historia ilipoanza Bajeti Kuu ya Serikali mwaka huu inasomwa mwisho, itapitishwa kwa pamoja pamoja na Wajumbe baada ya michango tofauti na pia kwa kuanzisha Kamati ya Bajeti ili kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu na yale mawazo ambayo Baraza hili wanataka kuyatoa yanaweza kufanyika kwa pamoja.

Mhe. Spika, nitaanza kwenda moja kwa moja kwenye suala la uchumi wetu. Uchumi wetu unakuwa kwa kasi na sifa hizi zimuendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na serikali yake kwa mambo mazuri wanayoyafanya. Lakini nataka

nizungumze mambo ambayo yanatugusa katika nchi moja kwa moja ambayo tumekuwa tunajipanga.

Kwanza nataka niongelee suala la uchumi au biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Biashara ya Tanzania Bara kuja Zanzibar mwaka 2015 ilikuwa bilioni 94.7, lakini mwaka 2016 kuna ongezeko la biloni 138 ambayo inaonekana kabisa fedha hizi na biashara imepanda. Lakini biashara ya Zanzibar kwenda Bara imepungua mwaka 2015 ilikuwa bilioni 401.3, lakini mwaka 2016 imepungua na kufikia bilioni 84.7 sawa mapungufu kwa asilimia 79. Sababu aliyosema Mhe. Waziri ni kuhusiana na sera ya biashara lakini pia mabadiliko ya masuala ya kodi.

Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa vya biashara na sisi kama Zanzibar wenzetu wanapopanga mikakati yao wanajipangia wao pia tumeangalia hata mwaka jana nilizungumza walipoleta *Finance bill* juu ya mabadiliko ya suala zima la ushuru. Walizungumza mambo mengi lakini moja ambalo sisi tunataka tulizungumze sisi Zanzibar ni njia gani ambayo na sisi tutaweza kulipanua soko letu kwa kuzingatia tunaweza kuingia katika soko la Tanzania Bara na Afrika Mashariki.

Nilitoa ushauri hapa nilipokuwa nachangia kwenye hotuba ya Wizara ya Waziri anayesimamia masuala ya Tawala za Mikoa jinsi ya kwamba sisi tuna wapiganaji wetu wengi na *main powers* na utaratibu wa kuangalia kuanzisha hizi *assembling plans* na kuanza kuzalisha bidhaa ambazo tutaweza kuuza katika soko la Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Nitakatoa mfano suala la *furnitures*. Kwa hivyo masuala haya hayahitaji nguvu nyingi wala hayahitaji akili nyingi yanahitaji mawazo kidogo, fikra na kuweza kuwatafuta watu ambao tunaweza kuunganisha nguvu, sheria tunazo za *public private partnership* kwa hivyo nikuunganisha nguvu zetu kuangalia wapi tunaweza tukapanda kwa pamoja.

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar bila ya Tanzania Bara au bila ya kuingia katika soko la Bara ni mtihani. Lakini pia hatuwezi sisi pia maisha yote tukawa tunategemea soko lao kwamba sisi pia kuwa wao wanatuletea bidhaa zao. Tuanze kujipanga na sisi katika maeneo ambayo tunaweza kufaidika. Katika MKUZA pameongelewa mambo matatu ambayo ni (*tourism)* utalii, (*business or trade*) biashara, pamoja na huduma *(services).* Mimi leo nataka nitoe ushauri kwa mara ya kwanza nasema tuweke vipaumbele vya mbali katika *strategy* zetu pamoja na hiyo MKUZA pamoja na hiyo MKUZA III na kuelekea dira ya miaka ya 2020 inayofuata kuangalia maeneo haya.

1) Tuanzishe (*ocean economy)* uchumi wa baharini;
2) *Tourism Industry* au Utalii
3) Tuunganishe *(service and trade)* biashara na huduma
4) Tufungue *oil and gas in economy*
5) Tufungue *agro-business* ambayo pia tuunganishe na *branding* ya Zanzibar ambayo tayari tumeshaanza kwa biashara zetu hasa katika masuala ya karafuu, *spices* na kutumia nguvu ya neno la Zanzibar katika mambo yote ambayo tunayataka.

Nataka niseme siyo lazima kwamba biashara utakayoisema *made in Zanzibar* ni lazima kiwe kinazalishwa Zanzibar. Unaweza uka *assemble product* hapa Zanzibar, utakatengeneza *hand bag* ukatengeneza viatu, ukatengeneza kofia, ukatengeneza suti kama hii niliyoivaa mimi na

ukaseme *made in* Zanzibar na ukauza nje. Cha msingi ni kuweza kulitumia neno la Zanzibar vizuri, hakuna eneo duniani utakapokwenda kote neno la Zanzibar ni ukweli kabisa Zanzibar ni maarufu kuliko Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda Ulaya ukimwambia mtu unatoka Tanzania anakuuliza Tanzania au Tasmania iko Australia, ukimwambia Zanzibar *Oh! I know Zanzibar*, atakutajia *Living stone* atakutajia *spices*, lakini bado neno la Zanzibar, kwanza neno hili la Zanzibar halina mwenyewe. Sisi kama serikali hatujalikamata sisi wenyewe, hatujalidhibiti. *Ownership* ya Zanzibar wanafaidika watu wengi sana nje ya nchi hii ambao wao ni Wazungu wanatumia neno la Zanzibar kwa sababu hili neno ni zuri lina historia na lina mvuto.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo ukiyaangalia duniani yaba mvuto kwa mfano Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein ana mvuto sio kama yule mwengine, ukimuangalia akipita Dkt. Shein wa Chama cha Mapinduzi ana mvuto. Kwa hivyo neno la Zanzibar lina mvuto kwa hivyo, lazima na sisi tujipange katika *branding* ya Zanzibar katika *products* tuwaangalie tutafaidika vipi. Tuacheni kuimba wimbo kila siku *branding* ya Zanzibar. Mimi sasa hivi zaidi ya miaka10 nakumbuka *branding* ya Zanzibar lakini kwa nini haliishi tukaona moja kwa moja leo tunaona *product* zote za *branding* ya Zanzibar. Katika hiyo mipango ya vipaumbele mtatengeneza fedha, mtaweza kuwavisha suti wananchi wote wa Zanzibar siku ya Sikukuu kama mtaweza kuifanya *branding* ya Zanzibar iwe sahihi. Hili halihitaji mawazo mengi wala ubunifu mkubwa ni kupanga mikakati mizuri kulitumia hili. Kwa hivyo mimi mimi naishauri sana serikali kwenye *branding* ya Zanzibar wajitahidi.

Mhe. Spika, juzi niliona Mhe. Makamu wa Pili aliongea na watendaji wake na Kiongozi mmoja kutoka Mauritius kuna mistari mizuri sana alitumia ile. Mimi naishauri sana serikali waitumie mikakati kama hii *forum* kama hizi kujifunza kwa wengine na naunga mkono juhudi kama hizi ili kuweza kupanua wigo na kufahamu vizuri, haya ni mambo ya msingi na sisi tunaweza kujifunza kwa wengine.

Mhe. Spika, nataka nizungumze katika *issue* ya visa na masuala ya utalii. Nimeshasema sana kuna *movie* moja inaitwa za *The Shaw shank Redemption* na kitabu chake pia kipo *The Morgan Freeman* ni muigizaji maarufu, huyu alikuwa amekaa kwenye *library* yeye ni mfungwa alikuwa anaomba atengenezewe *library* ya vitabu. Kwa hivyo alikuwa anaandika kwenye mamlaka husika kila mwezi anaandika barua moja, baada ya miaka 10 akaletewa *truck* moja vitabu akaambiwa kuanzia leo usitumie tena barua kwenye Halmashauri ili kuanzisha *library* kwa ajili ya vitabu ili wafungwa waweze kusoma.
European
Mhe. Spika, na mimi naomba nirudie katika Baraza lako tukufu sitochoka kusoma kutoa mawazo yangu kwa kile ninachokiamini japo kuwa majibu siyapati. Mimi bado naamini kama tutaondoa *visa fees* kwa ajili ya miezi ambayo ni ya *low season* tunayoita ambayo mimi sasa naiita ni ya *green season* ambayo siyo katika *European summer* ambayo ni Oktoba, Septemba na Novemba kwa wageni ambao watakuja *direct to Zanzibar* hasa kutoka Addis-Ababa kutoka Kenya, Ruwanda na Uganda kuja *direct to Zanzibar* tunaondoa *visa fees* siyo *visa* naamini kuliko vitanda vyetu sisi vikakaa vitupu tukaweza tukafaidika. Haina maana kwamba sisi tunapowawekea *tag* ZRB ambao wanajitahidi waweze kukusanya mapato lakini kitanda kinakaa kitupu. Kitanda kikaa kitupu unatumia fedha, unalipa mfanyakazi, lakini hakuna shilingi au dola

itakayoingia ndani ya nchi. Tutumie nafasi za kutumia nguvu na uwezo tuliokuwa nao bila ya kutumie fedha nyingi tutumie mawazo ili wageni waweze kumiminika kwa wingi.

Mhe. Spika, nataka niongee suala la ZIPA, katika ukurasa wa 124 cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia kuhusu mchango wa sekta binafsi. Sehemu ya 69 inasema:

> "Sekta binafsi kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010-15 Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar iliidhinisha jumla ya miradi 35 yenye thamani kadhaa."

Mhe. Spika, hii ndio ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo pia inatuongoza sisi kwenda mwaka wa 2020.

Mhe. Spika, nasoma kwenye *hansard copy* ambayo Mhe. Mwenyekiti ameisoma, hii ripoti ameisoma Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

> "Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar ZIPA, bado haijaweka mazingira mazuri kwa wawekezaji, mazingira ya kufanyia biashara Zanzibar bado ni magumu na hayamshawishi muwekezaji kuja kuwekeza. Hali hii inakwenda kinyume na matarajio yadira ya *vision* ya mamlaka hiyo na kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha kuvutia na ushindani wa kuekeza katika Kanda ya Kimataifa. Lakini pia Aidha ZIPA wameshindwa kutekeleza dhana ya *one stop center* ambayo Mhe. Hamza hapa ameizungumza kwa ndani pia na akaunganisha pamoja na Wizara ya Ardhi "

Sasa mimi niulize hii taasisi ya ZIPA ina malengo ya kukiumiza Chama cha Mapinduzi, kukirudisha nyuma Chama cha Mapinduzi. Kwa nini tunashindwa kuyafanya haya tunayoyataka ikiwa utalii ndiyo sehemu ambayo tunasema ni *bread and butter* sasa kwa nini tusitumie nguvu ya kubadilisha hii taasisi ili tukaenda mbele kabisa. Mimi nashauri sana Mhe. Waziri ZIPA ikiwa ni *hard beat* ya uchumi wetu basi ifanyike mageuzi ili tuweze kujua inatusaidia sisi pamoja na wawekezaji wetu wa ndani na wa nje.

Mhe. Spika, nataka nishauri kitu chengine inawezekana Wajumbe wa Baraza kuona mimi ninachoongea siyo sahihi. Mhe. Spika, naomba unilinde nasikia mazungumzo mengi Wajumbe hawawezi kunisikia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane kidogo, endelea Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, mimi nashauri kuna ubaya gani tukaanzisha *intensive training* ya lugha ya kiingereza mashuleni, kwa nini vijana wetu wanashindwa kujieleza kwa kiingereza vizuri. Lakini katika elimu hiyo baada ya kuweka Kifaranza tuweke na Kichina, tuanze kufundisha lugha ya kichina mashuleni. Umkute leo Mhe. Suleiman kutoka Chake Chake anazungumza "*niho chichopotu",* anaweza huyu na sisi wengine twende tukajifunze, tukenda tukapiga na sisi kichina. Wazanzibari sasa hivi tuanze kutoa wakalimani katika nchi za falme za kiarabu, kuwapeleka Marekani waweze kuongea Kichina.

Leo nilikuwa nasikiliza BBC namkuta Muingereza anaongeza kichina katika BBC *Radio World Service* asubuhi nimeshangaa nikasema hawa watu tuko nao karibu sisi, lakini leo nikiangalia humu ndani anayeongea kichina sina hakika ni nani labda viongozi waliokuwa katika mstari wa mbele. Lakini huku nyuma sisi sidhani kama kuna mtu anayeongeza Kichina na ukimkuta mtu anaongea kichina ni sifa. Mimi nashauri tuanzishe Kichina katika mashule yetu yote na kama sio lazima lakini iwe ni lugha ambayo inapewa kipaumbele. Mimi naamini Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China watatuunga mkono, wataleta walimu na watafanya kazi na sisi kwa ukaribu kabisa

Mhe. Spika, baada ya hapo nataka niongelee Baraza la Biashara. Baraza la Biashara limekufa hii ni sehemu ya *dialogue* baina ya *Public Private Partnership* waweze kuzungumza, lakini halijachukua hatua mpya kuna nini? Hii ni *forum* ya kipekee Bara wana TMBC na sisi tuna ZBC. Kwa hivyo mimi nashauri sana Baraza la Biashara liendelezwe, litiliwe *priority* katika suala zima. Mimi ningeshauri Baraza la Biashara alikamate Tume ya Mipango ambayo ni yule Mr. Juma Reli ili yeye katika dira nzima ya mipango pamoja na Wizara ya Biashara washirikiane kwa pamoja kuweza kusukuma hiyo sheria ya *Public Private Partnership* pamoja na ile *Condominium Act* ya 2010 ambayo hadi hivi sasa imelala ambayo sisi tuweze kuingia sasa hivi katika uwekezaji maarufu. Lakini sasa hivi miaka 7 sheria ya *Condominium Act* hakuna kitu tunachokiona tangu 2010.

Mhe. Spika, nataka niongelee katika Ilani ya suala la mafuta na gesi. Elimu ya mafuta na gesi iendelee kutolewa kila hatua ambayo serikali inachukua juu ya mikataba wanayofunga. Hatutopendelewa kusikia mambo kama yaliyowakuta Tanzania Bara katika masuala ya migodi yao. Mimi nataka tuulize masuala ya mafuta na gesi kama rasilimali ya Wazanzibari lakini pia hasa katika hizi *blocks* kutoka 12 mpaka unakuja kwenye 9 na 8 na pale panapofanyika *prospects* katika Tanga *basin* pamoja na *lather* ambayo inaitwa Kimbiji. Tuelezwe maelezo yote na katika mpango Waziri atakapokuja atupe hatua na mikataba aliyoifunga na kila hatua inayokwenda ili wananchi wamsikie na Waziri anayehusika elimu aendelee kuitoa katika vyombo vya habari kila mwezi ili kuhakikisha kuna *transparence* katika suala zima la la *oil and gas industries*.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka niongelee kwamba nashauri katika suala la kilimo. Ukenda kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye ukurasa wa 135 anazungumzia kuandaa mpango wa mazingira wa kuvutia sekta binafsi lakini pia katika uvuvi wa Bahari Kuu, utengenezaji wa boti za uvuvi, ujenzi wa vyumba vya baridi *(cold room),* pamoja na viwanda vya kusindika samaki.

Mhe. Spika, mimi katika Jimbo langu la Tunguu tuna mpango ambao namshukuru sana Mhe. Haji Omar Kheri, Waziri anayesimamia Tawala za Mikoa na Halmashauri zetu, kuniunga mkono katika soko la Kaebona. Mimi naamini baada ya kumalizika kwa barabara hii sasa hivi ya Cheju kuja mpaka Kaebona na kwa mpango mkuu ambao tayari serikali imeshatenga fedha kutoka Tunguu kuelekea mpaka Makunduchi kilimita 30 ambayo tayari mkandarasi ataanza kutafutwa katika miezi ijayo. Mimi naamini Kaebona itakuwa ni *center*, namuomba sana masuala ya kwenda kutoa vihori hivi kwa ajili ya biashara ya mwani pamoja na kujenga *cold rooms* tuelekeze nguvu katika eneo la Mkoa wa Kusini katika soko la Kaebona tutawasaidia wananchi kutoka Paje, Jambiani, Makunduchi, Kizimkazi, Uzi pamoja na Unguja Ukuu na Kikungwi na Bungi yenyewe yote kwa ujumla.

Hili kwa sababu tayari bandari ambayo inayotaka kutengenezwa katika upande wa Kizimkazi inaendelezwa. Si vibaya eneo la katikati tukaanzisha biashara ambayo pia tunaweza kutafuta tukaanzisha biashara tofauti ambazo zitakuwa ni za huduma kuweza kusogeza hasa moja kwa moja katika sekta ya kilimo kuweza kulihudumia eneo la Utalii na fuko kutoka Michamvi, Paje na Jambiani kwa upande wa Kaebona. Nimesema huko nyuma hakuna lazima wenye Mahoteli wa Mkoa wa Kusini kuja mpaka Mwanakwerekwe kununua vitu vya kilimo.

Mhe. Spika, nimeshakuona unataka kupiga kengele namalizia. Nataka niongelee masuala ya Bandari ya *Airport*.

Mhe. Spika, hakuna kisiwa chochote duniani kinachozungumzia masuala ya uchumi bila ya kuwa na *Airport* na Bandari njema. Bandari mimi nashauri katika eneo la bandari Mhe. Waziri husika aliangalie juu ya Bandari ya Bumbwini pamoja na Bandari ya Mpigaduri. Tuangalie tena bandari ipi itakuwa inatutosheleza sisi kwa upande wa Zanzibar, je twende Mpigaduri au Bumbwini. Ikiwa ni Bumbwini inawezekana basi tuangalie kwenye ilani tuweze ku-*revise* kwa sababu kina cha maji cha Bumbwini kinatosheleza, mazingira mazuri na pia tupo nje ya nchi tutaweza kutengeneza biashara na huduma na kuweza kuzalisha ajira nyingi zaidi. Mimi kwa upande wangu nashauri sana serikali iangalie juu ya Bandari ya Bumbwini kuliko Mpigaduri.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nikushukuru kwa kunipa nafasi, nimuombe pia Mhe. Waziri kuwa gazeti la Zanzibar leo sasa halifiki Tanzania Bara kutokana na kwamba linachapishwa Zanzibar, kwa hivyo sera ya serikali sasa itakuwa haifiki Bara. Wananchi wengi wanaulizia gazeti la Zanzibar leo kufika Bara. Nashauri *copy* 500 ziwe *printed* Zanzibar, 2000 ziwe *printed* Bara kwa hivyo gazeti litakuwa *printed* Zanzibar pamoja na Bara.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nikushukuru mimi naipongeza sana hii bajeti Mhe. Hamza Hassan ameiita ni bajeti ya matumaini. Mimi nasema hapana hii ni bajeti ya uhakika, serikali imefanya utafiti wako makini Serikali ya Chama cha Mapinduzi naunga mkono hoja mia juu ya mia na baada hapo Mhe. Spika, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said, Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona kwa mchana huu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kufika hapa leo tukiwa katika hali ya uzima lakini pia nikushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Baraza letu tukufu na vile vile kutuona UWAWAZA bila ya upendeleo.

Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja katika ukurusa wa 16 aya ya 33 Mfuko wa Miundombinu. Mfuko huu wa miundombinu una mambo mengi sana na mfuko huu tunasema kwamba ni mfuko mama kwa ajili ya miundombinu yote. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri bajeti yetu ya mwakani mfuko huu uweze kupewa kipaumbele zaidi kwa sababu tumeona kwa mwaka huu wa 2017 matatizo mengi ambayo yalijitokeza katika barabara zetu na mfuko huu pia unatumia ulipaji wa kuwalipa fidia wananchi wale ambao barabara zetu zimepita, kwa mara hii basi tuache lakini kwa mara ijayo naomba sana sana uongezewe bajeti yake.

Mhe. Spika, samahani vile vile niende katika ukurasa wa 21 aya ya 45 Mhe. Spika hapa tumeona kwamba wenzetu wa TRA wamejitahidi sana kuongeza mapato ZRB wamejitahidi sana tunawashukuru sana lakini pia nimwambie Mhe. Waziri kwamba wazee wetu wa zamani walisema kwamba "Mgema akisifiwa tembo hukilitia maji". Kwa hivyo nimuomba Mhe. Waziri akamate kamba yake madhubuti sana wala asijali kukatika kwa wengine wote watakaofanya ubadhirifu juu ya ukusanyaji huu wa mapato wa TRA na ZRB.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri hakusimama kidete kwa mwaka huu 2016/2017 basi tunamini kwamba haya mapato haya yasingeleweza kuzidi kwa kiwango kikubwa na tungelikuwa pale pale chini, lakini kwa umahiri wake na jitihada zake kubwa alizozifanya ndizo zilizosababisha kupanda kwa kiwango hiki. Kwa hivyo Mhe. Waziri jitahidi na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika marekebisho ya mishahara tunamshukru sana Mhe. Rais wetu kwa kuona kwamba iko haja ya wafanyakazi wake kuwapandishia mishahara hapa aliweka ahadi na tunaamini huyu ni kiongozi mahiri kwa nia safi kabisa ameweza kuitekeleza ahadi yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba unilinde Mhe. Spika muda wangu unapotea...

Mhe. Spika: Ahsante waheshimiwa tuendeleeni kumsikiliza Mheshimiwa.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika naamini kwamba marekebisho haya ya mishahara Mhe. Rais aliona pakubwa sana ndio akaweza kuongezea wafanyakazi mishahara hiyo, lakini pia tuwambie kwamba hawa wafanyakazi waliongezewa mishahara hii wameongezewa mishahara hii kwa matumaini ya kwamba watafanya kazi zao vizuri sana. Kwa hivyo tunaomba kwamba wafanye kazi na kwa kujali ile kazi yao sio wende pale wafanye kazi kwa maslahi tuu hapana kama wanataka kukiktumikia Chama cha Mapinduzi basi hii ndio sera ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 52 unaosema huu ndio uungwana na hivyo ndivyo vitendo vya Serikali ya Dk. Ali Mohamed Shein tunampongeza sana kwa juhudi zake na uungwana huu tunaamini kwamba utakuwa ni vigezo kwa Rais mwengine yoyote atakayekuja mbele yake, tunampongeza sana sana na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjalie maisha marefu.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika ulipaji wa deni la Tanesco. Ni jambo la kusikitisha sana ambalo tumelikuta wakati ule nilipokuwepo katika Kamati ya Mawasiliano tatizo hili lilkuwa ni kubwa na hili tatizo kwa kweli lilikuwa linakwenda danadana, lakini kwa jitihada walizozifanya au tulizozifanya Kamati ya Mawasiliano kuondoka hapa na kwenda Dar es Salaam kuonana na wenzetu wa Tanesco tulipata ukweli na ukweli ule ndio uliotusaidia na pia ukamsidia Mhe. Waziri kuweza kulitatua tatizo hili la Tanesco.

Kwa hivyo tunakuomba Mhe. Waziri ili kuweze kwenda sambamba na wenzetu usiwe na muhali kwa mtu yoyote kwa sababu muhali ndio unaozorotesha maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar. Tumechoka na wale ambao tuliwavumilia sasa hivi tuweze kufanya kazi nao bila ya kuwavumilia.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika mazingatio maalum ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar niseme kwamba Mhe. Spika, wale wote ambao hawataki mazingatio maalum ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar basi waondoke bila ya kuondoshwa waanze kuondoka wenyewe watupishie ili tuweze kufanya kazi vizuri na wale ambao wanaweza kuyakabili mazingiatio yote basi waweze kuyafuata.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar haitomuonea mtu lakini pia kwa wakati huu tulionao hatuko tayari kuyumbishwa kutokana na yale maazimio ambayo Serikali imeyaazimia. Serikali imeazimia kuwaletea wananchi wao maendeleo zaidi vijijini pamoja na mijini lakini na kuwaona vizuri wale wafanyakazi wote wa Serikiali hii tuliyonayo.

Mhe. Spika, mimi sitaki kusema mengi kwa leo kwa sababu mimi mwenyewe ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti lakini pia mengine tayari mengi nimeshayachangia kwa maandishi na niliona kwamba sitopata muda mzuri wa kutosha kuweza kuchangia sana.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yake makubwa aliyotupa wakati tulipokuwa tukiipitia bajeti hii, lakini mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chambani naunga mkono hutoba hii kwa asilimia mia moja.Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe nimebakiwa na wachangiaji wawili Mhe. Mussa Ali Mussa wa Ole na Mhe. Jaku Hashim Ayoub lakini muda tulionao haumtoshi hata mmoja nadhani kuchangia kwa hiyo nitawapa nafasi siku ya Jumatatu tukijaaliwa.

Lakini pia panapo majaaliwa siku ya Jumatatu baada ya wachangiaji hawa wawili tutakuwa na michango ambayo itakuwa inatoka kwa Waheshimiwa Mawaziri mpaka sasa hivi Mawaziri walioomba ni watano na Manaibu Mawaziri wawili baada ya hapo tena nitamwita mtoa hoja ili aweze kuja kuidhinisha hoja yake.

Baada ya tangazo hilo nina tangazo jengine Waheshimiwa Wajumbe mnaarifiwa kuhudhuria kwenye semina ya ZRB siku ya Jumapili tarehe 18 saa 3:00 za asubuhi katika ukumbi wa juu wa Baraza la Wawakilishi.

Baada ya matangazo hayo sasa naomba nihairishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 5:41 mchana Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 19/06/2017 saa 3:00 asubuhi)